
# Nipashe

Jumamosi Agosti 24, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581778
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**Fursa** tele zaja wazalishaji wa kahawa duniani wakikutana Dar

UKURASA 4



**Mwanafunzi** atiwa mbaroni madai ya kuhamasisha polisi wachomwe moto

UKURASA 5



**Mwinyi** aonya vijana dawa za kulevya, unywaji pombe uliokithiri

UKURASA 7



COURTOIS AKATAA KUICHEZEA UBELGIJI

UKURASA 21

# Utapiamlo mkali waua watoto, ma-DED kitanzini



• **Imebainika** hawakutenga fedha kuudhibiti, ripoti kutua kwa Samia aamue hatima yao... *Endelea uk. 15*



Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Dk. Samia Suluhu akiimba pamoja na vikundi mbalimbali vya askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wakati wakitoka kwenye zoezi la Medani katika shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 60 ya jeshi hilo, Pongwe Msungura, Msata, mkoani Pwani jana. **PICHA: IKULU**

# Rais Samia amaliza sakata la Ngorongoro

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3
SERIKALI YASHTUKA VIWANDA KUGEUZWA MAGHALA

UKURASA WA 9
ASKOFU ATOA ANGALIZO KWA VYAMA, WASIMAMIZI UCHAGUZI WA S/MITAA

UKURASA WA 15
WAFANYABIASHARA WATISHIA KUTUNZA FEDHA KATIKA CHAGA

## Viongozi dini, wadau watia neno utekaji

UKURASA 8

**MICHEZO** YANGA KUMALIZA KAZI MBELE YA VITAL O UK.24

**MAONI,** UK.6



Rais wa Zanzibar, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Waumini wa Dini ya Kiislamu, baada ya kumalizika kwa Ibada ya Swala ya Ijumaa katika Masjid Shura Magomeni, Wilaya ya Mjini Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# Rais Samia amaliza sakata la Ngorongoro

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza kurejeshwa huduma za kijamii kwa wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro iliyomo katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA).

Akizungumza na wananchi wa kata 11 zilizoko Tarafa ya Ngorongoro jana wakati akiwasilisha maagizo ya Rais Samia kwa wananchi waliokuwa wamekusanyika na kukesha kwa siku tano wakisubiri hatima yao, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri (Sera, Bunge na Uratibu), William Lukuvi, alisema:

"Mkuu wa Nchi ameagiza uchaguzi katika tarafa hiyo ufanyike kwa kutumia mipaka ya zamani, kama ulivyofanyika maeneo mengine.

"Mkurugenzi wa Ngorongoro, la mwisho aliloagiza Mheshimiwa Rais Samia hapa, hawa wananchi hakikisha wanapata huduma mbalimbali katika mamlaka hii, lakini zipo baadhi ya huduma hazitolewi vizuri, anayo habari.

"Kwamba kuna baadhi ya shule vyoo vyake vimeharibika, lakini ninyi hamvishughulikii. Kuna baadhi ya shule maji hayatoki, mashine zimeharibika hamzitengenezi. Kuna viongozi hapa wengine katika geti wanapata tabu kupita.

"Kuna watu wana magari. Hawa wenyeji wana magari yao, lakini wakati mwingine wanazuiwa kupita baada ya saa 10:30 jioni, ninakupa maelekezo haya Mkurugenzi wa Ngorongoro."

Lukuvi alieleza kuwa Rais Samia anawapenda watu wake kuliko yeye, hivyo hapendi usumbufu wowote; huduma za wanafunzi zitolewe kikamilifu, vivyo hivyo hospitalini.

"Ninataka mkuu wa mkoa uhakikishe kule kote huduma zilikositishwa na zilikuwapo kuhakikisha zinarejeshwa ili wananchi hawa wapate huduma.



"Vile vyoo ambavyo baadhi ya wanafunzi sasa tunayohabari wanajisaidia vichakani zijengwe wajisaidie katika maeneo yao," alisema.

Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema, "Nchi hii ni yetu sote, Watanzania wote tuko sawa, nchi hii imejengwa na Baba wa Taifa (Mwalimu Julius Nyerere) kuwa taifa moja, taifa la upendo, taifa la amani na taifa la umoja.

"Rais wetu Rais Samia anasimamia misingi hiyo hiyo, nchi ni moja, Watanzania ni wamoja, tuna haki sawa. Sisi sote Rais Samia ametutuma kwenu, mimi na kaka yangu William Lukuvi tuje kwenu, anawaomba muwe na amani na utulivu."

Waziri Kabudi aliwataka wawe na amani na upendo, huku akirejelea Ibara ya 8 ya Katiba, inayosema mamlaka yote ya serikali yanatoka kwa wananchi.

"Ninyi ni wananchi wa Tanzania na sehemu ya wanaoleta hayo mamlaka ya nchi. Ibara hiyo hiyo ya 8 inasema kazi kubwa ya serikali ni kuhakikisha ustawi wa wananchi.

"Rais Samia yupo kuhakikisha ibara hiyo ya Katiba inasimamiwa. Ibara hiyo hiyo inasema, wananchi wana haki kushiriki shughuli za nchi yao, na ninyi mna haki kushiriki shughuli za nchi yenu," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, alisema hatashiriki kukandamiza haki ya mtu mahala popote atapokuwa.

Alisema Rais Samia ambaye ni mwanadiplomasia mkubwa na mpenda amani anayetaka kila mtu aishi katika mazingira yake, naye anapenda haki.

"Sikuwahi kuja huku Ngorongoro, niliposikia kelele, sipendi kwenda mahali bila majibu. Hunibebi kama hakuna majibu na majibu yenyewe, lazima yawe na ukweli kwa sababu nitadaiwa mbele ya Samia na mbele ya Mungu wangu.

"Nisingependa niende mbele za Mungu nikumbushwe habari za Ngorongoro nilihusika kutenda udhalimu na kuumiza wananchi, hilo sitokubali, watu wengi wanapenda kutoa kauli bila kuyajua mambo," alisema.

Makonda alisema wapenda haki ni watu watulivu wanaotaka kujifunza na kusikiliza na kuchambua na kujua ukweli.

Juzi Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeeman Mbowe, aliishauri serikali kurudi katika meza ya mazungumzo na wananchi wahamishwe kwa ridhaa na ushawishi watakaopewa na si kutumia vyombo vya ulinzi na usalama kuwatisha.

## Othman aonya ufisadi kuvuruga amani, utulivu

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimesema amani na utulivu bila kuongozwa na dhamana ya pamoja kati ya viongozi, vyombo vya ulinzi na wananchi haiwezi kupatikana.

Kimesema dhima ya kulinda amani na utulivu haipatikani kwa mabilioni ya shilingi, bali kwa nia thabiti na dhamira ya wazi.

Mwenyekiti wa ACT Wazakendo, Othman Masoud Othman, ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZO, alitoa kauli juzi alipozungumza na waandishi wa habari visiwani Zanzibar.

Othman alisema msingi wa ustawi na kuwapo amani na utulivu hutokana na utashi wenye dhamira ya kweli katika usimamiaji masuala hayo na si kwa maneno yasiyo na vitendo vya wazi na kweli.

Alisema iwapo kila mmoja atakuwa tayari kutimiza wajibu wake kwa uadilifu na dhimira ya kweli, amani na utulivu vitapatikana bila kutumia nguvu au gharama yoyote.

Alisema kupatikana amani na utulivu hakuhitaji kupatiwa mkopo wa mabilioni au matrilioni ya shilingi au kuomba misaada toka nje kwa ajili ya ujenzi wa barabara, bali hujengwa kwa nia njema isiyo batili.

"Kila mmoja akitimiza wajibu wake kwa dhamira ya kweli na uadilifu, amani itapatikana. Amani hutanguliwa kwa nia, dhamira njema na uadilifu. Hujengwa pamoja na viongozi, vyombo vya ulinzi na wananchi," alisema.

Othman alisema amani haipatikani kama wanavyohangaikia kukopa ili kujenga barabara, shule na miundombinu, bali ni jambo mtambuka lenye manufaa ya pamoja.

Akizungumzia ufisadi unaotajwa Zanzibar, Othman alisema unafaidisha baadhi ya watu, huku akidai vitendo hivyo vinafahamika kwa vyombo vya dola.

"Hawataki mabadiliko kwa kuwa wanaona ufisadi ni biashara inayolipa na yenye tija. Wameshajua hakuna hatua zinazochukuliwa dhidi yao.

"Haya yote kimantiki ndio yanapelekea kuvuruga amani na utulivu Zanzibar. Ufisadi unaoendelea Zanzibar hakuna asiyeujua. Unafahamika na polisi, ZAECA na vyombo vya ulinzi," alisema.

Othman alisema wanaofanya ufisadi, "kubaka demokrasia" na kufanya dhuluma kama ilivyotokea mwaka 2020, hakitakuwa kigezo cha kuwabakisha madarakani mwaka 2025.

HABARI KITAIFA

## PM: Bila elimu vijana wetu hawatofika mbali

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewataka wazazi wahakikishe vijana wao wanakwenda kusoma kwenye shule za sekondari kwa kuwa bila elimu hawawezi kufika mbali.

"Wazazi wenzangu hakikisheni vijana wenu wanakwenda shuleni. Hatuwezi kufika mbali kama vijana wetu hawaendi shule. Tunajenga shule kila mahali, tunataka maeneo yote yawe na shule," alisema.

Mbunge huyo wa Ruangwa alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Mtondo, Kata ya Nambiranje, Ruangwa, mkoani Lindi.

Akielezea hatua iliyofikiwa kutokana na juhudi za serikali, Waziri Mkuu alisema Wilaya ya Ruangwa imepiga hatua katika sekta za elimu, maji na afya kulinganishwa na hali ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Alisema wilaya hiyo ina shule tatu za wasichana pekee ambazo ni Liuguru, Ruangwa Girls na Lucas Malia.

"Vilevile, tumefanikiwa kujenga shule za sekondari zenye kidato cha tano na sita ambazo ni Ruangwa, Mbekenyera, Nkowe, Lucas Malia na Hawa Mchopa. Shule ya sita ya Mandawa itakamilika hivi karibuni," alisema.

Akielezea utekelezaji kwenye sekta ya maji, Waziri Mkuu alisema vijiji vyote 90 vya wilaya vilichimbiwa visima kupitia taasisi ya GAIN lakini kwa sasa hayatoshi.

Hata hivyo, alitumia fursa hiyo kuwajulisha kwamba serikali imetoa Sh. bilioni 49 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji kutoka Nyangao ambao utavinufaisha vijiji 34 vya Wilaya ya Ruangwa na vijiji 29 vya Wilaya ya Nachingwea.

Kuhusu umeme, Majaliwa alisema laini zimeshakwenda kwenye kila kijiji na kwamba serikali hivi sasa inashughulika kuweka umeme ngazi ya vitongoji.

Kuhusu barabara, Majaliwa alisema kuna changamoto ya barabara kufika katika Kijiji cha Mtondo ambayo tayari iko kwenye mpango wa ujenzi.

"Kuna barabara ya kutoka Mandawa Chini hadi hapa, Nanjalu hadi hapa, Nambiranje hadi hapa na kutoka Namiyenje hadi hapa," alisema.

Awali Diwani wa Nambiranje, Mossa Mtejela alimwomba Waziri Mkuu awasaidie ili waongezwe fedha za ujenzi wa barabara ya kutoka Mtondo hadi Mkaranga Sekondari yenye urefu wa kilometa saba kwa kuwa kuna daraja linapaswa kujengwa na fedha iliyotengwa ni Sh. milioni 300 tu.

Waziri Mkuu anaendelea na ziara jimboni kwake.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo (katikati), akiwa katika ziara ya kutembelea viwanda mbalimbali, mkoani Tanga jana, kuangalia maendeleo na kusikiliza changamoto zao. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Rais Samia aahidi neema JWTZ

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Samia Suluhu Hassan amesema atasimamia shabaha ya kuwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) madhubuti na lenye maofisa na askari wenye weledi, ari na zana bora.

Aliyasema hayo jana wakati akifunga zoezi la Medani katika kuadhimisha Miaka 60 ya JWTZ katika eneo la Pongwe Msungura, lililoko Msata.

Rais Samia alisisitiza kuwa jeshi imara zaidi litatokana na dhamira ya kweli, moyo wa kujituma na uchumi imara zaidi.

Vilevile, Amiri Jeshi Mkuu aliitaka JWTZ kuendelea kulinda misingi ya kuanzishwa kwa jeshi hilo na kuendelea kudumisha nidhamu, utii, uaminifu na uhodari uliopo katika jeshi hilo.

Rais Samia pia alisisitiza JWTZ kuendelea kuwa Jeshi la Wananchi la ukombozi la mfano kwa Afrika na dunia kwa namna linavyooonesha uhodari, weledi na nidhamu ya kijeshi.

Mkuu wa Nchi pia alishukuru Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa kushirikiana na JWTZ katika zoezi la Medani lililojumuisha mazoezi ya baharini na nchi kavu.

Pia alipongeza ujio wa meli kubwa ya hospitali ya kijeshi iliyotoa huduma ya vipimo na matibabu kwa wananchi takribani 8,000.

Kupitia mazoezi hayo, JWTZ imebadilishana uzoefu kuhusu mbinu mbalimbali za kupambana na ugaidi, uvuvi haramu, uharamia, usafirishaji haramu wa watu na dawa za kulevya.

# Serikali yashtuka viwanda kugeuzwa maghala

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo amekuwa mkali kwa wafanyabiashara waliochukua viwanda wakati wa ubinafsishaji na kuvigeuza kuwa maghala.

Amesema kuwa, hali hii imewakosesha ajira Watanzania, akielekeza viwanda hivyo vifufuliwe.

Amesema wizara yake kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji na Msajili wa Hazina, imejipanga kuhakikisha viwanda hivyo vinafufuliwa na kuanza kazi mara moja, ili viweze kuwa na mchango katika uchumi.

Waziri Jafo alitoa kauli hiyo jana akiwa ziarani mkoani Tanga ambako alitembelea viwanda na kuzungumza na wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda kwa lengo la kujionea utendaji kazi, kusikiliza changamoto zao na kuona njia bora ya kuzitatua kwa kushirikiana na taasisi zingine husika.

Katika ziara hiyo, waziri huyo aliagiza Wakala wa Vipimo (WMA) kukagua mita zote za umeme viwandani ili kuhakikisha zinafanya kazi kwa usahihi na wazalishaji, wafanyabiashara, walaji na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wanapata haki yao kwa usawa.

"Mkoa wa Tanga kuna viwanda vinavyofanya vizuri na vingine havifanyi vizuri, hivyo sijaridhishwa na watu waliochukua viwanda wakati wa ubinafsishaji, lakini havifanyi kazi.

"Ninawashauri wawekezaji waliochukua viwanda vilivyobinafsishwa kwa nia ya kuwekeza wawekeze na si kuvigeuza kuwa maghala au kuwa sehemu ya kupata mikopo na kuwaacha Watanzania wakikosa ajira na nchi ikikosa mapato," alielekeza.

Waziri Jafo alisema kuwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Wizara ya Fedha, Msajili wa Hazina pamoja na taasisi za kisekta, atahakikisha changamoto zilizotolewa, zinafanyiwa kazi ili kurudisha hadhi ya Mkoa wa Tanga kuwa mkoa wa viwanda kama ilivyokuwa wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza.

Kuhusu changamoto ya umeme mdogo, Waziri Jafo alisema serikali imefanya jitihada kubwa kushughulikia hilo na kwamba Mradi wa Kufua Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) uko mbioni kukamilika, hivyo tatizo hilo litatatuliwa. Katika ziara hiyo, Waziri Jafo alitembelea Kiwanda cha Sabuni cha Wilmar Tanzania Limited, Kiwanda cha Nguo cha AFRITEX, Kiwanda cha Maziwa cha Tanga Fresh, Kiwanda cha Unga cha Pembe Flour Mills na Kiwanda cha Saruji Kilimanjaro.

Akiwa katika Bandari ya Tanga, Waziri Jafo alipongeza upanuzi wake na kutoa wito kwa watumishi kurahisisha usafirishaji mizigo ya wafanyabiasha wa ndani na nje ya nchi kwa ufanisi ili kuvutia wawekezaji.

Alisema bandari hiyo ikiwa na ufanisi itavutia watu kuanzisha viwanda mkoani humo na wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi kutumia bandari kusafirisha bidhaa mbalimbali kama magari, madini ya copper na mazao, hususani katani na nyinginezo.

Waziri Jafo aliwaahidi wawekezaji kuwa atashirikiana na taasisi zingine za kisekta kutatua changamoto zao ili kuhakikisha kila sekta ya viwanda na biashara inayoajiri watu wengi na kuchangia katika ukuaji wa uchumi, inafanya kazi kwa ufanisi na kuleta mandeleo ya kijamii na ya kiuchumi.

Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Jafari Kubecha, alisema kutokana na maboresho ya mazingira ya biashara yanayofanywa na serikali, ikiwamo upanuzi wa bandari, viwanda vitafufuliwa na biashara mkoani humo itakuwa inachangia kwa kiasi kikubwa katika ongezeko la ajira na Pato la Taifa.




Mkurugenzi wa Bodi ya Kahawa (TCB), Primus Kimaryo akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa kongamano na maonesho ya 21 ya Kahawa Bora za Afrika linalotarajiwa kufanyika kuanzia Februari 26 hadi 28 mwakani. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Dk. Mwinyi aahidi kuboresha madrasa, maslahi ya walimu

**Na Mwandishi Maalum,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema kuna haja kwa serikali kuangalia kwa karibu miundombinu duni ya madrasa, maslahi ya walimu wa madrasa na maimamu wa misikitini.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar wakati wa mazungumzo na viongozi wakuu na wajumbe wa Baraza la Ulamaa Zanzibar waliofika kumtembelea.

Alisema miundombinu ya madrasa, maslahi ya walimu wa madrasa na maimamu wa misikitini nchini ni dhaifu mno, hivyo ni vyema serikali kwa kushirikiana na vyombo vya kidini kuangalia njia nzuri ya kufanya kazi na kusaidia kuzitatua changamoto hizo.

Akizungumzia mmomonyoko wa maadili katika jamii, Dk. Mwinyi alisifu juhudi za baraza hilo kwa kuendelea kutoa elimu kwa jamii licha ya tatizo hilo kuwa kubwa.

Pia alipongeza uongozi na wajumbe wa baraza hilo kwa jitihada zao za kutoa elimu ya ndoa kwa wanandoa na warajis wa ndoa Unguja na Pemba ili kupunguza matatizo na migogoro ya ndoa katika jamii sambamba na kutoa fatwaa (uamuzi kulingana na misingi ya dini ya Kiislamu) kutokana na changamozo zinazoikabili jamii.

Kuhusu migogoro mbalimbali inayohusiana na dini ya Kiislamu kwenye jamii, Alhaj Dk. Mwinyi alipongeza baraza hilo kwa weledi wa utatuzi mzuri wa migogoro hiyo, sambamba na kutatua hata viashiria vinavyosababisha migogoro hiyo.

Vilevile, Rais Dk. Mwinyi hakuacha kulisihi baraza hilo kuendelea kuisimamia amani na utulivu kwa kutumia lugha moja kupitia viongozi wao, maimamu misikitini pamoja na wanasiasa kwenye majukwaa yao ili kuendeleza taifa lenye umoja na mshikamano.

Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaab, alipongeza juhudi za maendeleo anazozisimamia Alhaj Dk. Mwinyi hasa kwa kipindi kifupi cha uongozi wake.

Alimwahidi Rais kumpa ushirikiano wa hali ya juu kutoka kwa baraza hilo kupitia misingi ya Quran, hadithi, fikhi na tafsiri pamoja na kufuata miongozo na sunnah za Mtume (S.A.W) hasa kwenye suala zima la kusimamia ustawi, amani na utulivu wa nchi.

Awali akizungumza kwenye kikao hicho, Katibu Mtendaji kutoka Ofisi ya Mufti Zanzibar, Sheikh Khalid Ali Mfaume, alisema miongoni mwa kazi za baraza hilo mbali na kumshauri na kumsaidia Mufti Mkuu wa Zanzibar, pia wanatoa elimu kwa walimu wa madrasa, wanandoa na warajis wa ndoa kwa kuwakabidhi vibali baada ya kuhitimu mafunzo, kutatua mambo mbalimbali ya dini ikiwamo kutoa fatwaa kwa matatizo yanayoikabili jamii.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455 Mtaa wa Mtumba,
Fax: +255 26 2323233 S.L.P. 2888, 40470 DODOMA
Barua Pepe: ps@mow.go.tz Tovuti: www.mwtc.go.tz

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumatatu tarehe 26-08-2024 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Kilombero** kupitia **Mikumi,** gari hilo lina namba ya usajili: **T 204 DYJ / T 572 EAZ**

   Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 28.00
   Upana - mita 5.20
   Kimo - mita 4.35

2. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam**, hadi Kilombero **kupitia Mikumi**, gari itasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

# Fursa zaja wazalishaji kahawa duniani wakikutana Tanzania

**Na Joseph Mwendapole**

WAZALISHAJI na wadau wa kahawa zaidi ya 2,000 kutoka mataifa mbalimbali duniani wanatarajiwa kukutana jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujadili maendeleo ya biashara hiyo na kupeana mbinu za kuiboresha.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Chama cha Kahawa Bora Afrika (AFCA), Amir Hamza, wakati wa uzinduzi wa Kongamano na Maonyesho ya 21 ya Kahawa Bora za Afrika litakalofanyika kuanzia 26-28 Februari mwakani, jijini Dar es Salaam.

Alisema kongamano na maonesho hayo ni jukwaa kubwa zaidi la biashara ya kahawa barani Afrika, ambalo huvutia zaidi ya wadau wa kahawa 2,000 kutoka ndani na nje ya Afrika kila mwaka.

Hamza alisema kongamano hilo hukutanisha wazalishaji, wafanyabiashara wa kahawa, wakaangaji kahawa, wadau kutoka sekta ya umma na binafsi na wawakilishi wa serikali.

Alisema kongamano na maonesho hayo yatafanyika nchini kwa mara nyingine baada ya kufanyika kwa mara ya mwisho mwaka 2016.

"Tanzania ni nchi yenye fursa kubwa katika katika sekta ya kahawa na kongamano na maonesho haya yanadhihirisha ubora wa kipekee wa kahawa za Afrika na pia yanaimarisha dhamira ya nchi za Afika kukuza ukuaji na ushirikiano katika sekta ya kahawa Afrika.

"Kaulimbiu ya Kongamano la 21 ni 'Kuhuisha Ongezeko la Thamani' ambapo kwenye kongamano hilo patakuwa na orodha ya wazungumzaji maarufu kimataifa na kikanda," alisema Hamza.

Alisema maonesho ya kahawa yatakayofanyika, yataonesha ubunifu na maendeleo yaliyotokea hivi karibuni katika sekta ya kahawa.

Alisema kutakuwapo pia warsha ambazo zitakuwa na majadiliano yenya tija, kutoa fursa za kipekee za kuonja na kutathmini kahawa na safari maalum zitakazoandaliwa ili kujifunza kuhusu kahawa.

Alisema kuwa katika kongamano na maonesho hayo, kutakuwa na mashindano ya watayarisha kahawa Afrika na mashindano ya kahawa bora katika ukanda wa Afrika ili kuonesha vipaji na bidhaa bora zaidi za kahawa kutoka kote barani.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya JJAD Kagera Farmers Ltd, Dk. Albert Katagira, alisema wanamshukuru kipekee Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusaidia bei ya kahawa kupanda kutoka Sh. 1,200 mwaka jana mpaka kufikia Sh. 5,300 kwa kilo.

Kampuni ya JJAD Kagera Farmers Limited iliyoko wilayani Kyerwa, mkoani Kagera, imekuwa inaendesha kilimo cha kahawa aina ya Robusta katika mashamba yenye ekari 100.

"Zao la kahawa kwa mwananchi wa Kagera sasa limekuwa mkombozi mkubwa na ninashukuru sana AFCA kuamua kuleta kongamano na maonesho ya kahawa Tanzania mwakani.

"Kongamano hilo litatusaidia sana kuongeza mbinu mpya za kulima zao hili na tutapata masomo mengi," alisema Dk. Katagira.

Aliomba serikali ione umuhimu wa kukopesha wakulima wa kahawa kwa kuwa kuandaa mashamba ya zao hilo ni gharama kubwa.

"Kuendesha mashamba makubwa ya kahawa si kazi rahisi, hivyo tunaomba serikali ione umuhimu wa kuwa inakopesha wakulima mikopo midogo ya kulima kahawa ili wakulima wengi wahamasike kulima zao hili," alisema.

Mkurugenzi wa Bodi ya Kahawa (TCB), Primus Kimaryo alisema kongamano la 21 litakalofanyika mwakani na ni fursa ya kipekee kwa wakulima wa kahawa kwa kuwa uzalishaji kahawa umekuwa ukiongezeka.

Alisema Bodi ya AFCA iliamua kuwa kongamano lao la mwakani lifanyika jijini Dar es Salaam na itakuwa fursa ya kipekee kwa wakulima wa kahawa Tanzania kuonesha kahawa wanayozalisha kwa ajili ya kutafuta masoko ya zao hilo.

"Hii ni fursa kubwa kwa wakulima kutafuta masoko ya kahawa na kuongeza ubora wa kahawa kwa sababu bei ya kahawa duniani inazidi kuwa nzuri, hi v y o wanapaswa kuitumia hiyo fursa kuyafikia masoko ambayo ni makubwa," alisema.

# Mwanafunzi atiwa mbaroni madai kuhamasisha polisi wachomwe moto

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linamshikilia Mwanafunzi wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Kanda ya Ziwa, Elias Anania (20) kwa tuhuma za kuhamasisha vurugu kupitia kundi sogozi la WhatsApp.

Inadaiwa mwanafunzi huyo amewataka wenzake kununua petroli na kuchoma askari polisi wenye sare popote watakakokutana nao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Wilbroad Mutafungwa, alidai kuwa mbali na kuhamasisha askari kuchomwa moto, pia aliwataka wachome moto watumishi wa umma. Alisema kijana huyo anadaiwa kusambaza ujumbe katika kundi hilo, akishawishi wenzake kununua petroli na vibiriti kushambulia askari wa jeshi hilo.

"Anashikiliwa kwa tuhuma za uchochezi, katika kuhamasisha hivyo, alidai kuwa vijana wamechoka, hivyo anawahimiza kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya maslahi yao na kudai haki zao za msingi," alisema.

Kamanda Mutafungwa alisema mtuhumiwa huyo anaendelea kuhojiwa na uchunguzi utakapokamilika atafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.



Waliokuwa askari polisi wakiwa chini ya ulinzi wa askari magereza, baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi inayowakabili ya wizi na kutishia kwa kutumia silaha, ambayo imefikia hatua ya ushahidi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# DC ajitosa migogoro ya ardhi vijijini

**Na Agustino Kihombo**

WANANCHI wa vijiji vya Makatapola na Mbweleli, Kata ya Migoli, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, mkoani Iringa, wameomba serikali kuingilia kati mgogoro wa mipaka unaokabili vijiji hivyo na kuhatarisha usalama wao.

Wananchi wa vijiji hivyo wamekuwa wanategemea kilimo na ufugaji kuendesha maisha yao, lakini wamejikuta hatarini kuingia katika mapigano baina yao kutokana na changamoto ya mipaka inayotenganisha Kijiji cha Mbweleli ambacho wananchi wengi ni wakulima, huku Kijiji cha Makatapola kikikaliwa na wafugaji wengi.

Wakizungumza mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Kheri James aliyefika katika vijiji hivyo juzi kusikiliza changamoto zinazosababisha kuibuka kwa mgogoro huo, walisema licha ya serikali kuweka mipika n kuainisha maeneo kwa ajili ya kilimo na ufugaji, wafugaji wameendelea kupeleka mifugo katika maeneo yao huku wafugaji nao wakiwalalamikia wakulima kuvamia maeneo ya malisho ya mifugo.

Agripina Thomas na Fredy Mapangala ni baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Mbweleli waliosema kumekuwa na vipigo kutoka kwa wafugaji huku wengine wakiumizwa pale wanaokutwa katika mashamba yao, jambo lililoongeza hofu kwa wananchi wa Mbweleli na kushindwa kufanya shughuli za kilimo kwa uhuru wakihofia kuumizwa na wafugaji.

"Sisi wananchi wa Kijiji cha Mbweleli hatujawahi kupigana na mtu ila tunapigwa na wafugaji wanapotukuta katika mashamba, wanatupiga na kutuumiza tukiwa ndani ya mipaka yetu, tunaomba serikali itulinde, tunaumizwa na wafugaji," walilalama wananchi hao.

Hoja hiyo ikaungwa mkono na Mwenyekiti wa Mbweleli, Michael Kitulo ambaye alisema katika eneo ambalo wananchi wake wamekuwa wakipigwa, ni sehemu ya maeneo ambayo serikali ya kijiji hicho inayatambua kama maeneo ya wakulima, hivyo amekuwa akishangazwa na vitendo vinavyofanywa na baadhi ya wananchi wa kijiji jirani.

"Eneo ambalo tunagombania na wenzetu ni eneo tulilolitenga kwa ajili ya wakulima, wote tunatambua hivyo, sijui kitu gani kimetokea hadi wafugaji wanaingiza mifugo yao na kuwapiga wananchi wangu, kiukweli mkuu wa wilaya hali si shwari, watu wanatishwa na kupigwa kwenye eneo la kijiji chao na mipaka ipo, tunaomba serikali tusaidieni ili amani iendelee kuwapo," alisema Kitulo.

Alipoulizwa kuhusu suala hilo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Makatapola, Merej Sungura alisema haamini kama kuna mgogoro wa mipaka baina ya kijiji chake na kijiji jirani kwa kuwa ndio walioongeza mipaka zaidi ya mara moja kutoka kwenye eneo lake.

Alisema wataalamu wa ardhi walifika katika vijiji hivyo na kuweka mipaka rasmi, lakini wanashangazwa na wanakijiji jirani kuhitaji mpaka mwingine tena nje na ule wa awali uliowekwa.

"Kwa kweli inashangaza sana kuona watu wanainuka na kusema tuna mgogoro, lakini uhalisia hapa hatuna mgogoro kwa sababu mimi na serikali yangu ya kijiji tuliwaongezea eneo hawa hawa wanaosema tuna mgogoro kwa zaidi ya mara moja.

"Leo tena wanasema eneo lao halitoshi, kitu ambacho si kweli. Ninachojua lipo eneo ambalo lilitengwa kwa ajili ya malisho milimani, wanalitaka kwa ajili ya kilimo, ndiyo maana wanaomba eneo lingine," alisema Sungura. Baada ya kusikiza hoja za pande zote mbili, Mkuu wa Wilaya ya Iringa James alitoa maelekezo kwa maofisa ardhi kufika na kujiridhisha kuhusu mipaka inayolalamikiwa.

"Ninaloliona hapa ni suala la mpaka tu, hakuna mgogoro hapa. Kwa kuwa GN ipo na wataalamu wapo, ninatoa siku tatu maofisa ardhi waje wapite kwenye mpaka mwanzo mpaka mwisho wabaini nani anaishia wapi na anapakana wapi na wawaoneshe viongozi wa vijiji ili kila mmoja ajue mpaka wake na mkishajiridhisha mimi nitakuja hapa nitoe majibu ya serikali na nini cha kufanya baada ya hapo," alisema mkuu wa wilaya.

Kuhusu wafugaji kujichukulia sheria mkononi kwa kuwapiga na kuwaumiza wakulima, Mkuu wa Wilaya alitoa onyo kali kwa yeyote atakayejihusisha na vurugu hizo, huku akisema ni kosa la jinai kujihusisha na mapigano ya aina yoyote ndani ya wilaya yake.

Alisema hakuna mtu mwenye ardhi na mwenye haki ya kumdhuru mwingine kwa namna yoyote ile kwa mujibu wa sheria za nchi.

## 'NGO zisiwe kichaka cha kuharibu maadili'

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama ameyataka mashirika yasiyo ya kiserikali kutokutumika kama kichaka cha kuleta mmomonyoko wa maadili katika jamii, bali yafanye kazi kwa kuzingatia maadili na kudumisha mila na tamaduni za Kitanzania.

Mboni Mhita alitoa angalizo hilo jana wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa mashirika hayo uliofanyika wilayani Kahama na kuhudhuriwa na zaidi ya mashirika 40.

Mboni alisema mashirika hayo yanapaswa kuwa wadau muhimu katika kuimarisha utawala bora na kupambana na vitendo viovu vinavyodhalilisha utu na mila na desturi za Watanzania.

Alisema umoja wao ni msingi unaowaunganisha na kuleta maendeleo endelevu kwa taifa.

Mwenyekiti wa Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali Wilaya ya Kahama, Bakari Kibile alisema mashirika hayo yanafanya kazi kwa kuzingatia kanuni, sheria na taratibu na yamesajiliwa kwa afua tofauti, zikiwamo za utunzaji mazingira, afya, kusaidia waraibu wa dawa za kulevya, uwezeshaji mabinti kiuchumi, elimu, kilimo, utawala bora na haki za binadamu.

Kibile alisema kuwa pamoja na mchango mkubwa unaotolewa na mashirika hayo katika jamii, yanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa rasilimali watu, fedha na watalamu wa kuandika miradi, hali inayopelekea mashirika mengi kufanya kazi kwa kusuasua.

Alisema mashirika mengi yamekuwa yanategemea rasilimali fedha kutoka kwa wafadhili, hivyo pale fedha za wafadhili zinapokosekana, yanasitisha shughuli za kusaidia jamii.

Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (TAKUKURU), George Japhet, alisema fedha za wafadhili zisipotumika kwa malengo yaliyokusudiwa, husababisha kuweka taswira mbaya kwa shirika katika jamii na kuonekana kama vikundi vya wapigaji.

Akitoa elimu ya kodi kwa mashirika hayo, Ofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Kikodi Kahama, Jaliwa Wilson, aliyataka mashirika hayo kulipa kodi kwa mujibu wa sheria isipokuwa kwa mashirika yenye msamaha wa kodi kutoka kwa Kamishna wa mamlaka hiyo.

Alisema kuwa baadhi ya mashirika yamekuwa yanatoa huduma na kufanya biashara, hivyo yanapaswa kulipa kodi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga mna deni kwa Rais Samia Suluhu

**WIKI** hii inayomalizika kesho imekuwa ya aina yake kwenye medani ya michezo hapa nchini, hususani soka.

Kumekuwa na shughuli nyingi za michezo ambapo Ligi Kuu Tanzania bara imeendelea lakini kitu kingine ni uwepo wa tamasha la kila mwaka la Kizimkazi linalofanyika visiwani Zanzibar.

Katika tamasha hilo wakati wa uwekaji jiwe la msingi ujenzi wa kituo cha michezo cha Suluhu Akademi, Rais Samia Suluhu Hassan alitoa taarifa njema kwa klabu zetu kubwa, Simba na Yanga.

Rais Samia alidokeza kuwa lipo jambo linaloendelea kwa ajili ya klabu hizo ambazo mara kwa mara wamekuwa wakiiwakilisha nchi kwenye mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la soka Afrika, CAF.

Rais Samia akizungumza kwenye hafla ya uwekaji jiwe la msingi wa kituo hicho, alisema amefanya mazungumzo na wadau na wawekezaji wakubwa hapa nchini kwa ajili ya kuzisaidia klabu hizo kongwe.

"Najua wadhamini au washika vilabu hivi wanafanya jitihada kubwa sana, lakini pamoja nao nimeongea na wadau, wawekezaji wetu wakubwa hapa, mmoja nimempa Yanga, mmoja nimempa Simba awasaidie," alisema Rais Samia.

Hili ni jambo zuri na la kupongezwa kwa Rais wa nchi kuona umuhimu wa kuziongezea nguvu klabu hizi ili ziweze kufanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa.

Ingawa bado mambo hayajakamilika na wadhamini hawajatangazwa, lakini pindi itakapokamilika, klabu hizi zijue zina deni la kulipa kwa Rais Samia katika kuonesha shukrani kwa kuongezewa wadhamini.

Nizikumbushe klabu zetu hizi, shukrani pekee na yenye kumbukumbu nzuri ni kuhakikisha mara baada ya mchakato mzima kumalizika, basi zijipange kufanya vizuri zaidi kwenye mashindano ya kimataifa.

Rais ameona juhudi za klabu hizi katika kutafuta wadhamini iliwachangie kufanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa, ameona kuna haja ya kuzisaidia kupata wadhamini wengi zaidi ili safari yao ya kufanya vizuri kimataifa iwe nyepesi.

Tunampongeza Rais Samia kwa jambo hili, lakini tunazikumbusha klabu hizi kuhakikisha zinajipanga vizuri mara baada ya kupata wadhamini hao wafanye vizuri zaidi kimataifa.

Ni wazi kwa sasa klabu zetu hizi kucheza hatua ya robo fainali mashindano ya kimataifa, iwe Ligi ya Mabingwa Afrika au Kombe la Shirikisho ni jambo la kawaida, zijiandae kumpa shukrani Rais kwa kuvuka hatua hiyo.

Lakini jambo lingine la kumpongeza Rais Samia ni ujenzi wa kituo cha michezo cha Suluhu Akademi kule Kizimkazi, ni wazi kituo hicho kikikamilika kitawapa nafasi na fursa vijana kukuza na kuendeleza vipaji vyao.

Ujenzi wa kituo hicho umejumlisha ujenzi wa viwanja mbalimbali vya michezo, ni jambo kubwa katika maendeleo ya michezo hapa nchini.

Tanzania ili kufikia ndoto ya kufanya vizuri siku moja katika mashindano mbalimbali, ni lazima tuwe na vituo kama Suluhu Akademi vingi zaidi ili kutoa fursa vijana wadogo kuanza kukuza na kuendeleza vipaji vyao.

Wito wetu, Watanzania watumie vizuri kituo hicho kuendeleza vipaji ili Tanzania izalishe vijana wengi mahiri kwenye michezo mbalimbali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Hongera TPBL kusikia kilio udhamini timu zaidi ya moja

**ILIANZA** kama mzaha. Ilianza minong'ono pembeni juu ya mdhamini mmoja kudhamini timu zaidi ya moja kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wadau wanajua soka ni mchezo wa 'fair play', hivyo haitakiwi kuwe na maswali kuhusu haki na usawa kwenye michezo mbalimbali.

Wengi walijikita juu ya Kampuni ya GSM kudhamini zaidi ya timu moja, ambapo wamekita mizizi yake kwa Yanga, huku pia ikiwa na udhamini kwenye klabu zingine za Ligi Kuu.

Wadau hao wa soka wakaenda mbali sana wakasema huko Ulaya, hata kampuni ambayo haijajiweka wala kuwa na timu haiwezi kudhamini timu zaidi ya moja kwenye ligi ya nchi moja.

Mfano, Arsenal, Real Madrid zinadhaminiwa na kampuni moja, lakini ni kwa sababu zipo nchi mbili tofauti.

Kampuni hiyo imeruhusiwa kudhamini timu moja tu nchini England na hairuhusiwi kufanya hivyo katika timu nyingine nchini humo, ndiyo maana ikaenda kudhamini kwenye nchi nyingine.

Sababu ni kwamba kama kampuni hiyo ingedhamini zaidi ya timu moja nchini England, mwisho wa siku ingeweza kuamua au kusimamia matokeo ya timu moja ambayo wao wanaweza kuiteua.

Mfano timu zilizodhaminiwa na kampuni moja zikakutana, halafu moja inahitaji ushindi ili asishuke daraja au inataka kuchukua ubingwa, sidhani kama itakosa pointi tatu.

Ni kwa sababu kampuni inayozidhamini itaweka mkono wake kuhakikisha timu yake moja haishuki daraja kwa ajili ya kuendelea kutangaza, au kupata ubingwa ili kuendelea kukuza nembo yake.

Kwa wenzetu jambo hili wanalichukulia kwa uzito sana, na wenzetu hawafichifichi juu ya uwezekano na timu kupanga matokeo kutokana na kuwa zipo kwenye jamii moja.

Baadaye ukawa mjadala mkubwa kwenye vyombo vya habari, televisheni, redio, vijiwe vya soka na mitandao ya kijamii juu ya kuwa hakuna usawa wowote kwa GSM kudhamini klabu zingine huku timu yake mama ikiwa ni Yanga.

Wakasema angalau hata ingekuwa kampuni huru kama ile ya ndege iliyokataliwa Ulaya kudhamini timu zaidi ya moja, lakini ukweli usiopingika kwamba huwezi kuitenganisha GSM na Yanga.

Kampuni hiyo ndiyo inayoisaidia klabu kuleta makocha, kulipa mishahara ya wachezaji na mambo mengi kadha wa kadha.

Hatujawahi kusikia GSM akilipa mishahara Pamba Jiji, Coastal na timu zingine, ina maslahi na Yanga kuliko klabu zingine.

Mjadala huo mkali ukamuibua Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo ambaye amesema amesikia mijadala hiyo na kuahidi kuifanyia kazi.

"Hizi siku mbili tatu umekuwa mjadala mkubwa, lakini kwa wakati huu tuliokuwa nao hakuna kanuni inayozuia kampuni moja kuweza kudhamini zaidi ya timu moja.

Udhamini ni jambo la kikanuni, madhumuni ya kanuni kwa asilimia 90, yameelekezwa kwenye klabu husika, wachezaji, waamuzi, viongozi, mbali na mijadala iliyoibuka, hakuna klabu yoyote au mdau kuelekea msimu huu, aliyelalamikia hilo kuona kama jambo hilo lina ukakasi," alisema Ofisa Mtendaji huyo.

Hata hivyo, alisema kanuni siyo msahafu, hivyo kama wadau wataona kuna haja ya kuja na kanuni hiyo, milango iko wazi.

Lakini mimi siku zote nimekuwa nikiamini kuwa kanuni siyo msahafu, zinajadilika, zinabadilishika kwa hiyo pale ambapo wadau wataona kuna haja ya kufanya mabadiliko ya kanuni kama ambavyo siku zote tumekuwa tukifanya.

Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF) na Bodi ya Ligi, sisi ni wasikivu mara zote na ndiyo maana unaweza, ukaona zoezi ambalo lina uwazi na ushirikishwaji mkubwa ni eneo la maboresho ya kanuni kuelekea kwenye msimu mpya jambo ambalo linafanyika katika kila msimu," alisema.

Tunaipongeza TFF na Bodi ya Ligi kwa kuahidi kulifanyia kazi suala hilo na kuonekena ni kweli viongozi wapo kwa ajili ya soka na si maslahi binafsi ya mtu mwingine.

Ni kweli suala hili linatakiwa kufanyiwa kazi kwa sababu hata kama hakuna chochote kinachofanyika, lakini kuweka kanuni tu kwa ajili ya chochote kibaya kinachoweza kutokea huko mbele na kuwepo kuaminiana kati ya klabu moja na nyingine zinazoshiriki Ligi Kuu, pia kuiamini kuwa bingwa wake anapatikana kihalali.

HABARI KITAIFA

## Wapewa elimu ya fedha kuepuka mikopo umiza

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Kilombero, Dustan Kyobya amepongeza wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara, wilayani Kilombero kwa kuwa na nidhamu na mikopo waliyochukua na kuirejesha kwa wakati.

Kyobya alitoa pongezi hizo wakati akifungua programu maalum ya Elimu ya Fedha kwa Umma inayoendeshwa na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na washirika mbalimbali wa sekta ya fedha nchini iliyofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Maendeleo – Ifakara, mkoani Morogoro.

“Kinamama mpo vizuri sana katika kurejesha mikopo mnayochukua na ndio maana uchumi wa wanawake katika mji wa Ifakara unakua kwa kasi kulinganishwa na vijana ambao wamekuwa na tabia ya kutorejesha mikopo yao kwa wakati,” alisema Kyobya.

Aliongeza kuwa ili kupata maendeleo ya haraka, ni vyema watu wakope kupitia taasisi zilizoidhinishwa na Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania.

Alisema kuwa kwa kufanya hivyo wataepuka changamoto mbalimbali zinazotokana na wakopeshaji wasio rasmi ambao wamekuwa wakiwaingiza wananchi kwenye hatari ya kufilisiwa mali zao.

Mkuu wa Wilaya aliwataka wananchi wa Halamshauri ya Mji wa Ifakara kitumia vizuri fursa ya elimu ya fedha waliyoipata ili iwasaidie kutatua changamoto wanazokutana nazo kupitia mikopo hasa ile inayotolewa kwa masharti magumu na mikataba isiyoeleweka inayoandaliwa na baadhi ya watoahuduma za fedha nchini.

“Ninajua kuwa mna changomoto kubwa mnayopitia kwa watoahuduma za fedha wasio waaminifu kwa kuwapa mikataba iliyoandaliwa kwa lugha ya Kiingereza, wakati wengi wenu hamfahamu lugha hiyo.

“Na kuna mtoahuduma za fedha mmoja nilishamfukuza wilayani kwangu kwa kusumbua wananchi na mikopo yake isiyoeleweka,” Kyobya alisema.

Alipongeza serikali kwa kuamua kutoa elimu ya fedha hasa kwa wananchi wa vijijini, na kuongeza kuwa kutokana na fursa nyingi za kilimo zilizopo Kilombero, elimu hiyo itanufaisha wananchi wa wilaya hiyo katika kuongeza uzalishaji mazo ya kilimo na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Kyobya aliagiza maofisa maendeleo ya jamii wa Wilaya ya Kilosa kuhakikisha wanaratibu mafunzo ya aina hiyo, yafanyike mara kwa mara katika kata zote wilayani Kilombero ili kutatua changamoto zinazokabili wananchi wa wilaya hiyo kuhusu mikopo umiza.

Programu maalum ya elimu ya fedha kwa maeneo ya Mkoa wa Morogoro inalenga kuhimiza wananchi kujiwekea akiba katika taasisi rasmi za fedha kama vile benki ili kuwa na fedha kwa ajili ya shughuli za kilimo badala ya kutumia fedha zote na kwenda kukopa mikopo umiza wakati wa kilimo.

# Dk. Mwinyi aonya vijana dawa za kulevya, unywaji pombe uliokithiri

**Na Mwandishi Maalum,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaji Dk. Hussein Ali Mwinyi ameitaka jamii kuweka mkazo kwenye malezi ya vijana na watoto ili kuwanusuru na mmomonyoko wa maadili.

Alhaj Dk. Mwinyi alielekeza hayo jana wakati akitoa salamu baada ya kujumuika pamoja na waumini wa dini ya Kiislamu kwenye sala ya Ijumaa, Msikiti Shuraa ulioko Magomeni, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema kumekuwa na mmonyoko mkubwa wa maadili na vitendo viovu vinavyosababishwa na vijana wanaojihusisha na matumizi ya dawa za kulevya na unywaji pombe uliokithiri.

Alihimiza wazazi kuhakikisha vijana wanapata elimu ya dini kwa ajili ya kujitambua na kujiepusha na vitendo viovu.

Alhaj Dk. Mwinyi alisema Zanzibar ilikuwa nchi yenye sifa na kusimamia maadili lakini yameporomoka kutokana na matumizi ya dawa za kulevya kwa kundi kubwa la vijana.

Rais pia alihimiza viongozi wa dini kuendelea kuhubiri na kuhimiza waumini kufuata misingi ya dini ili kuirejesha nchi katika maadili mema.

Awali Katibu Mtendaji wa Ofisi ya Mufti Zanzibar, Sheikh Khalid Ali Mfaume alishauri watumiaji wa vileo kufikiria madhara ya mihadarati wanayotumia badala ya kufikiria starehe ya muda mfupi.

Sheikh Khalid alisema dini ya Kiislamu imekataza matumizi ya pombe kwa kufahamu athari zake kwa mtumiaji na jamii na kusisitiza vijana kurudi katika misingi ya dini ili kujinusuru.



Mratibu wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa utendaji kazi askari polisi wa Dawati la Jinsia na Watoto mkoa wa Kipolisi wa Ilala, Mkaguzi wa Polisi Dk. Christina Onyango, akisisitiza jambo kuhusu kampeni ya ‘Tuwaambie Kabla Hawajaharibiwa’ ya kunusuru wanafunzi dhidi ya ukatili wa kijinsia, wakati wa mafunzo hayo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# CRDB yatoa msaada wa samani shuleni

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

BENKI ya CRDB Tawi la Tunduru imekabidhi viti na meza 40 katika Shule ya Sekondari Kungu, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma.

Akikabidhi vifaa hivyo jana, Meneja wa CRDB Kanda ya Kusini, Denis Mwoleka kwa Kaimu Ofisa Tawala wa Wilaya ya Tunduru, Abdalah Luzaga, alisema vifaa hivyo vina thamani ya Sh. milioni tatu.

Mwoleka alisema ugawaji vifaa hivyo ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali kutoa huduma ya elimu bila malipo kwa Watanzania na kurudisha fadhila kwa jamii, pia shukrani kwa wana Tunduru ambao wameendelea kupata huduma zao katika benki hiyo.

Akipokea vifaa hivyo, Kaimu Katibu Tawala huyo pamoja na kushukuru Benki ya CRDB alisisitiza viongozi wa shule kusimamia utunzaji na matumizi sahihi ya vifaa hivyo.

Alihimiza vifaa hivyo vikawe chachu ya ufaulu kwa wanafunzi wa shule hiyo.

KABWELA NA FADHILI MOHAMED





Wafanyabiashara wadogo, wakisubiri wateja wa bidhaa zao, chini ya daraja la juu la magari, eneo la Ubungo Dar es Salaam jana, eneo ambalo si rasmi kwa shughuli hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Viongozi wa dini watoa neno utekaji

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya viongozi wa dini wameshauri serikali kufanyia kazi hoja ya watu kupotea, kuteswa na kutekwa ili kuondoa hofu inayoendelea kujengeka katika jamii.

Huku wakiwa na maoni tofauti kuhusu hoja ya kuundwa tume ya Rais ilivyopendekezwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) juzi, viongozi hao wamesema kuna haja serikali kuchukua hatua dhidi ya matukio hayo.

Viongozi hao wamesema zimeshaundwa tume nyingi katika nyakati tofauti, lakini hazijaleta matokeo na kumwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuviagiza vyombo vyake vya ulinzi na usalama kutoa taarifa sahihi kuhusu matukio hayo.

Juzi, Mbowe alimwomba Rais Samia kutumia mamlaka yake kwa mujibu wa Sheria ya Uchunguzi Mahsusi ya Mwaka 2019, kuunda Tume ya Kimahakama ya Majaji kuchunguza tuhuma za matukio hayo.

Wakizungumza jana na Nipashe kwa nyakati tofauti, viongozi wa dini, akiwamo Mwenyekiti wa Madhehebu ya Kikristo Mkoa wa Dodoma, Askofu Antony Mlyashimba, walisema wanaunga mkono kauli ya Mbowe kutaka serikali kuunda tume hiyo ya uchunguzi.

"Ipo haja serikali kuunda tume ambayo itafanyia uchunguzi suala hili ili kuondoa hofu kwa wananchi hasa wakati huu wa kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani.

"Kama serikali itaendelea kukaa kimya, basi hofu hii ya wananchi itawafanya hata kushindwa kushiriki uchaguzi wenyewe kwa kuhofia usalama wao.

"Kutokana na wengi wanaotekwa kuwa wa upinzani, basi watu wanaweza jenga dhana potofu kuwa serikali inataka kuharibu uchaguzi," alidai.

Askofu Mlyashimba alisema serikali ifanye uchunguzi na kuja na majibu ambayo yatafanya wananchi kujua ni watu gani ambao wamekuwa wakihusika katika vitendo hivyo vya kuteka watu.

Askofu wa Kanisa la International Evangelism (IEC), Thadey Selyvester, alisema kuwa kama hali hiyo haitafanyiwa kazi na serikali hivi sasa, hata kampeni za vyama vya siasa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, watu hawatashiriki kutokana na hofu ya matukio ya utekaji.

"Ninaomba serikali kufanyika kazi jambo hili ili wananchi wake waishi kwa amani na uhuru badala ya kuendelea kuwa na hofu kama ilivyo sasa ambapo watu wanaishi kwa shaka," alisema.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Elim Pentecoste Tanzania (KEPT), Peter Konki alisema utekaji unaosemwa na wananchi ukiendelea kufumbiwa macho utamchafua Rais Samia, wakuu wa mikoa na wilaya, hivyo ni vizuri serikali ifanye uchunguzi kubaini watekaji hao.

Konki alisema jambo likisemwa na watu zaidi ya mara 10, linakuwa lina ukweli, si la kukaa kimya, ni la kukemea ili lisiendelee.

Alisema ni vizuri serikali za mitaa na vijiji ikaweka ulinzi wa kutosha kwa watu wake bila kusubiri polisi ambao ni wachache.

Alitumia fursa hiyo kuitaka jamii kuripoti wageni wanaoingia mitaani ambao hawajulikani ili kupata uhalali wao kama ni watu wema au wahalifu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maaskofu na Mashehe ya Haki Amani na Maadili kwa Jamii ya Madhehebu ya Dini nchini, Askofu William Mwamalanga, alisema kuunda tume ya kijaji kuchunguza matukio ya utekaji na kupotea kwa watu si suluhu.

Alisema kama ni tume, zimeshaundwa nyingi katika nyanja mbalimbali, lakini hazijaleta matokeo kinachotakiwa Rais Samia aviagize vyombo vyake vya ulinzi na usalama kutoa taarifa sahihi kuhusu matukio hayo.

"Mpaka sasa serikali ilipaswa iwe imefanya utafiti na uchunguzi wa kina wenye majibu yaliyoshiba ya nani anateka watu.

"Kinachoshangaza ukimya wa serikali katika hili unaashiria nini? Maana yake imeshindwa kutimiza wajibu wake wa ulinzi kwa wananchi.

"Kuna taarifa kwamba kuna watu wengine wanafuatiliwa kila wakati, jambo kama hili ni baya sana kwa nchi, hiki kikosi kimetoka wapi cha kuteka watu na kuwapoteza?" alihoji Askofu Mwamalanga.

Alisema serikali inatakiwa kutoa taarifa ya ukweli kwa wananchi, kuunda tume ni kama inaficha wajibu wake, inatakiwa ijue makundi ya kuteka watu katika nchi yanatoka wapi.

Alisema hatari nyingine anayoona yatajitokeza makundi ya watu yatakayoua yatakayoteka raia na lawama itakuwa kwa serikali kutokana na ukimya wake wa kutokemea vitendo hivyo kwa nguvu.

Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria wa Chama cha ACT-Wazalendo, Mbarala Maharagande, alisema tume inaweza kusaidia kupata ufumbuzi.

"Sisi tumekuwa na mapendekezo ya kulifumua Jeshi la Polisi na kulijenga upya na kusimamia mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai iliyoundwa na Rais ambayo yangeweza kusaidia kuboresha mifumo ya utendaji wa jeshi hilo.

"Jambo lingine ni mitaala mbalimbali ya kijeshi ibadilishwe ili wasitumie mabavu katika kuendesha shughuli zao za kila siku," alisema.

Julai 15 mwaka huu, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Camillus Wambura, alisema Jeshi la Polisi halihusiki na matukio yanayodaiwa kuwa ni ya utekaji, kwa kuwa jukumu la msingi na la kikatiba la jeshi hilo ni kuhakikisha linalinda usalama wa raia na mali zao.

IGP Wambura alitoa kauli hiyo wakati akiwa mkoani Simiyu akiendelea na ziara yake ya kuzungumza na maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali.

***Imeandaliwa na Jaliwason Jasson (MANYARA), Paul Mabeja (DODOMA) na Halfan Chusi (DAR)**

# Tanzania Mwenyekiti Mkataba wa Nairobi utunzaji mazingira

**Na Robert Hokororo**

TANZANIA imechaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Nairobi kuhusu utunzaji mazingira wakati wa Mkutano wa 11 wa Nchi za Ukanda wa Magharibi mwa Bahari ya Hindi uliofanyika Antananarivo, Madagascar.

Hatua hiyo itaifanya Tanzania kuwa nchi mwenyeji wa Mkutano wa 12 (COP 12) wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Nairobi.

Akihutubia mkutano huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji juzi, aliahidi kuendeleza ushirikiano na nchi zingine wanachama katika kuendeleza, kusimamia na kutunza mazingira ya bahari kwa ukanda huo.

Alishukuru wanachama wanaoingia Mkataba wa Nairobi kwa kuichagua Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Ofisi ya Mkataba wa Nairobi na kusema kuwa hiyo ni heshima kubwa ambayo itaenziwa.

"Hii ni COP yangu ya kwanza (tangu nilipoteuliwa) lakini ninahisi kama nimekuwapo kwa muda mrefu kwa sababu ya kukaribishwa na ninyi nyote na namna mada ngumu zimefanywa rahisi na kueleweka kwa wasio wataalamu," alipongeza.

Waziri huyo aliahidi kuwa Tanzania itafanya chochote kilicho ndani ya uwezo ili kuhakikisha uamuzi uliopitishwa katika COP 11 unatekelezwa kwa mafanikio na sekretarieti inafanya kazi kwa ufanisi.

Dk. Kijaji ambaye aliambatana na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Immaculate Semesi na wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, alisema kupitia uzoefu wa mkutano huo, Tanzania itahakikisha inakuwa na mkutano wa COP12 bora zaidi.

Mkutano wa Mkataba wa Nairobi ulifunguliwa Agosti 20 hadi 22, 2024 ambapo Dk. Kijaji alifanya mikutano ya pembeni na viongozi mbalimbali kujadili mikakati ya mazingira.

Miongoni mwa washiriki aliofanya nao mazungumzo kwa nyakati tofauti ni pamoja na Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), Elizabeth Mrema, Mshauri wa Kiuchumi wa Mradi wa Western India Ocean Initiative, Brenda Kibiki na Msimamizi wa Programu ya Lead Blue Economy – Western India Ocean (WIO) kupitia Mradi wa The Nature Conservancy (TNC), Dk. Tuqa Jirmo.



# Vyama, wasimamizi wapewa angalizo Uchaguzi wa Mitaa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

UMOJA wa Madhehebu ya Kikristo mkoani Dodoma, umevitaka vyama vya siasa kujikita kutangaza sera zao kwa wananchi badala ya kukashifiana na matusi.

Mwenyekiti wa Umoja huo, Askofu Anthony Mlyashimba alisema hayo jana wakati anazungumza na waandishi wa habari jijini hapa, akivitaka vyama hivyo vyenye usajili kuhakikisha vinatumia kampeni zao kunadi sera zao na si kukashifiana na kutoa lugha chafu.

Askofu huyo pia alitaka vyama vya siasa kuhakikisha vinapitisha wagombea wenye maadili ya kiroho na wanaokubalika na jamii ili watakapochaguliwa, watatue changamoto za wananchi bila kujali itikadi za vyama vyao.

"Watanzania wanatarajia wagombea watakaoteuliwa na kupitishwa na vyama vyao vya siasa, wawe watakaosaidia jamii na serikali katika kuleta maendeleo bila kujali atakayemwongoza anatoka kwenye chama gani cha siasa," alisema.

Kiongozi huyo wa kiroho pia alitaka wasimamizi wa uchaguzi kutoa haki na kuzingatia sheria, huku wakitoa elimu kwa wapigakura wakati wanapojaza fomu badala ya kusubiri makosa yafanyike na kuwakosesha haki yao.

Alisema wasimamizi wa uchaguzi wakitumia nafasi zao hizo kuelimisha wagombea na wapigakura inaweza kuondoa changamoto ambayo ilijitokeza kwenye uchaguzi wa mwaka wa 2019 ambao Watanzania walio wengi walionekana hawajui kusoma na kuandika.

"Tunataka wasimamizi hao wa uchaguzi wasiwe marefa na makocha wa chama kimoja, bali wawe marefa na makocha kwa vyama vyote vya siasa na wasimame kwa pande zote. Hii itasaidia kutopindisha sheria na malalamiko kutoka kwa Watanzania," alisema.

Pia aliomba viongozi mbalimbali wa kiroho, wakiwamo maaskofu, mashehke, wachungaji wainjilisti na mapadri kutumia nafasi zao kuhamasisha waumini wao kujitokeza kwenye maeneo yao kugombea katika uchaguzi huo.

# Mpango aonya mawaziri kujifungia ofisini

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango amewaagiza mawaziri wote wa kisekta kuacha kukaa ofisini, badala yake wafanye ziara za vijijini, kubaini shida zinazokabili wananchi.

Amesema ni lazima miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa ikamilike kwa wakati na kwa thamani inayotakiwa na iwapo itacheleweshwa, hatua nyingine zitachukuliwa.

Dk. Mpango alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ziara yake ya siku nne mkoani hapa iliyolenga kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo.

Akiwa wilayani Mpwapwa katika majimbo ya Kibakwe na Mpwapwa, Makamu wa Rais aliwataka mawaziri wa kisekta kuwa na utaratibu wa kufanya ziara maeneo ya vijijini, ili kubaini changamoto za wananchi pamoja na kuzipatia ufumbuzi.

"Ninapenda kuagiza watendaji wote wa serikali kuhakikisha mnafanya kazi kwa kushirikiana kwa kutatua kero za wananchi na msiwe watu wa kukaa maofisini kwa kusubiri taarifa," alisisitiza.

Dk. Mpango pia alimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Waziri wake, kuhakikisha wanamaliza changamoto ya maji ambayo inawakabili wananchi wa Halmashauri ya Mpwapwa.

Alisema si sahihi wananchi wa halmashauri hiyo ambayo ni wilaya kongwe kuendelea kupata changamoto ya maji mpaka sasa.

Kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika mwezi Novemba na Uchaguzi Mkuu mwakani, Dk. Mpango alisisitiza Watanzania kutofanya makosa -- wachague viongozi wenye uchungu na maendeleo badala ya wachumiatumbo.

Pia aliagiza Waziri wa Maliasili na Utalii na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kufika Mpwapwa kwa ajili ya kufanya mipango ya matumizi ya ardhi katika eneo la Milima ya Wota, ambako kuna uharibifu mkubwa wa mazingira.

Alisisitiza kuwa suala la utunzaji mazingira lizingatiwe katika mlima huo ambao wananchi wake wamekuwa wakifyeka misitu kwa ajili shughuli za kilimo.

"Hatuwezi kuharibu nchi namna hii kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira," Makamu wa Rais alionya.

Kuhusu elimu, Dk. Mpango aliagiza watoto wenye umri wa kupelekwa shuleni, wazazi na walezi wahakikishe wanawaandikisha na kufuatilia maendeleo ya walioko shuleni.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dustan Kitandula, alisema maeneo yenye misitu yamekuwa na uharibifu wa mazingira na kusisitiza lazima yahifadhiwe kisheria na wananchi kulinda uoto wa asili.

Kitandula alisema watatoa mizinga 200 kwa vikundi vya vijana ili wafuge nyuki kwa ajili ya kipato na kutunza mazingira.

Alisema ufugaji nyuki ni fursa kubwa kwa sababu soko la China linahitaji tani milioni 38 za asali kwa mwaka.

Naibu Waziri huyo alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa serikali yake kutoa Sh. bilioni saba kwa ajili ya wilaya hiyo ambapo kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 32 zimepelekwa Kibakwe.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akizungumza na wananchi na viongozi mbalimbali katika Kijiji cha Mpwayungu, Jimbo la Mvumi, wakati akihitimisha ziara ya kikazi ya siku nne, mkoani Dodoma juzi. **PICHA: OMR**

# Wataka utafiti wanaofanya vibaya ukusanyaji ushuru

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

MADIWANI wa Halmaahauri ya Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida, wamewataka maofisa kilimo kufanya utafiti katika kata zinazofanya vibaya katika ukusanyaji ushuru wa mazao, ili kujua aina ya mazao yanayopaswa kulimwa katika kata hizo kwa lengo la kuongeza mapato.

Waliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani ambacho kilikuwa maalum kwa ajili ya kujadili mapato ya halmashauri hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ally Mwanga, alisema baadhi ya kata zimekuwa zinafanya vibaya katika ukusanyaji mapato kila mara, hali ambayo imekwamisha maendeleo katika halmashauri hiyo.

Alisema watendaji lazima watambue kuwa mapato ndio kitovu cha maendeleo ya halmashauri na kuwaomba walifanya vibaya kujitahidi kudhibiti mianya ya utoroshaji mazao nyakati za usiku.

Madiwani hao walisema kuna umuhimu wa kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kutokutegemea vyanzo vya msimu wa kilimo pekee, mfano minada, vivutio mbalimbali na vibanda vya biashara katika maeneo kama vituo vya mabasi.

Walisema vyanzo hivyo vikianzishwa na kusimamiwa vizuri, vitaongeza mapato ya halmashauri na kutumika katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, aliwaelekeza watendaji wa kata na vijiji kushirikiana kwa karibu, ili kukusanya mapato ya halmashauri kikamilifu na kuziba mianya ya utoroshaji mazao katika maeneo korofi.

"Tupo tayari kutoa motisha kwa kata zinazofanya vizuri katika ukusanyaji mapato, ili kuhamasisha ukusanyaji katika kata zinazofanya vibaya, zifanye vizuri zaidi," alisema





# Watalii waongezeka Zanzibar, Italia yaongoza kuleta wageni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMLA ya wageni 68,223 wameingia Zanzibar kwa mwezi Julai, 2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.2 kulinganisha na wageni 58,711 walioingia mwezi Julai 2023.

Ofisa Utafiti na Utalii kutoka Kamisheni ya Utalii, Hassan Ameir Vuai, aliyasema hayo jana alipowasilisha takwimu za uingiaji wageni kwa mwezi Julai mwaka huu.

Vuai alisema kuwa kwa kulinganisha na wageni 51,559 kwa mwezi Juni 2024, kuna ongezeko la asilimia 32.3.

Alisema nchi ya Italia ndiyo iliyoongoza kwa kuleta jumla ya wageni 7,703 sawa na asilimia

11.3 ya wageni wote, ikifuatwa na Ufaransa iliyokuwa na wageni 5,442 (sawa na asilimia nane).

Alisema Uingereza ni ya tatu kwa kuingiza wageni 5,090 (asilimia 7.5) huku Ujerumani ikishika nafasi ya nne kwa kuingiza wageni 4,587 (sawa na asilimia 6.7) na ya tano ni Poland iliyokuwa na wageni 4,519 sawa na asilimia 6.6.

Vuai alisema jumla ya wageni 45,293 waliingia nchini kutoka Bara la Ulaya sawa na asilimia 66.4 huku Bara la Afrika likifuata kwa kuwa na wageni 8,638 sawa na asilimia 12.7.

"Bara la Asia lilikuwa la tatu kwa kuwa na wageni 8,022 sawa na asilimia 11.2 na Oceania ilikuwa na wageni 731 sawa na asilimia (1.1)," alisema.

Vuai alisema wageni 60,178 sawa na asilimia 88.2, waliingia Zanzibar kupitia viwanja vya ndege na wageni 8,045 sawa na asilimia 11.8, waliingia kupitia bandarini.

"Wageni 34,818 (asilimia 51) walikuwa na jinsia ya kiume na wageni 33.405 (asilimia 49) ni wa jinsia ya kike. Asilimia 99.1 ya wageni walikuja nchini kwa ajili ya mapumziko, huku asilimia 0.5 walitembelea ndugu na marafiki na asilimia 0.4 waliingia kwa ajili ya sababu nyinginezo kama biashara na mikutano," alisema.

Meneja Msaidizi- Uchumi Benki Kuu Tawi la Zanzibar, Shami Chamicha, alisema kutokana na kukua kwa sekta ya utalii, hali ya uchumi wa nchi inaendelea kuimarika na hali ya wananchi inabakia katika njia sahihi.

Ofisa Uhusiano Idara ya Uhamiaji Zanzibar, Shariff Bakar Shariff, alisema idara hiyo imeimarisha huduma zake ikiwamo mifumo ya kielektroniki kwa kuwezesha wananchi na wageni kuomba visa kwa urahisi zaidi.

Alisema huduma hiyo imesaidia kuepusha usumbufu kwa waombaji ndani na nje ya Zanzibar.

# Daktari Bingwa ashauri wananchi kujitokeza katika kambi za matibabu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

DAKTARI Bingwa wa Upasuaji ameomba wananchi kutumia fursa ya kambi za madaktari bingwa zinapotangazwa kwa kujitokeza kwa wingi ili kupatiwa matibabu ya kibingwa.

Dk. Rashid Masoud Said alitoa ushauri huo jana alipozungumza na waandishi wa habari visiwani hapa kuhusu kambi ya upasuaji wa maradhi mbalimbali ya wiki moja iliyofanyika katika Hospitali Kuu ya Mnazimmoja, ikiendeshwa na madaktari wazawa.

Alisema wananchi wanapofika katika kambi za matibabu za namna hiyo, hujihakikishia huduma za kibingwa zinazotolewa sambamba na kupata ushauri kulingana na hali za afya zao.

Alisema kambi hiyo ililenga kufikia wananchi waliohitaji upasuaji wa maradhi mbalimbali, ikiwamo ngiri za watu wazima na watoto, kuondoa vijiwe katika nyongo na magonjwa mengine.

Alitaja huduma nyingine zinazotolewa ni upasuaji wa matundu madogo kupitia utaalamu wa madaktari bingwa wa Kichina ambao wamekuwa wanasaidia kutoa utaalamu wao kwa madaktari wazawa.

"Tunashukuru kambi hii imekwenda vizuri na ulikuwa upasuaji maalum wa njia ya matundu. Njia hii ni bora badala ya kumpasua mgonjwa tumbo lake, imekuwa rahisi baada ya ujio wa madaktari wa China," alisema.

Dk. Said alisema kuwa awali upasuaji ulikuwa haufanyiki kwa wingi na ulichukua muda mrefu, lakini baada ya mafunzo ya madaktari hao, madaktari wazalendo wamejifunza na sasa wanaufanya.

Aliwatoa hofu wananchi kuhusu aina hiyo ya upasuaji, akieleza kuwa hivi sasa huduma hiyo ndiyo inayotolewa zaidi katika mataifa yaliyoendelea.

Dk. Said aliishukuru timu ya madaktari wa China, ambao wamesaidia kupanua wigo wa uelewa wa kitaalamu kwa madaktari wazawa.

Kiongozi wa timu ya madaktari 33 kutoka China, Prof. Jiang Guoqing, alisema wamefurahishwa kuona madaktari wazawa wanafanya vizuri katika upasuaji wa kutumia matundu madogo, jambo ambalo linaleta faraja katika ushirikiano wa nchi hizo mbili.

Prof. Jiang Guoqing alisema timu ya madaktari wa China iliamua kuimarisha mafunzo kwa madaktari wa upasuaji katika ufundi wa upasuaji wa kutumia darubini, ili kuwajengea uwezo wa kutoa huduma bora kulingana na ukuaji wa sayansi na teknolojia.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa Zanzibar, Riziki Pembe Juma (kulia), akisisitiza jambo alipotembelea kampuni ya AE Q kukagua maendeleo ya ukarabati wa makazi ya wazee, eneo la Sebuleni Unguja, juzi. Kushoto ni Meneja wa kampuni hiyo, Bakari Abdalla na (nyuma) ni Meneja wa mradi huo, Abeid Ben. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtakwimu aanika hali ya biashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

THAMANI ya biashara kwa mwezi Julai mwaka huu imeonesha nakisi ya Sh. bilioni 139.1, ikipungua kwa asilimia 10.7 kulinganishwa na Julai 2023 na imeongezeka kwa asilimia 16 kulinganisha na mwezi uliopita wa Juni.

Mtakwimu Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Sharih Khatib Faki, aliyasema hayo wakati akiwasilisha takwimu za biashara za kimataifa kwa mwezi Julai huko Mazizini, mjini Unguja jana.

"Uwiano wa usafirishaji na uagizaji kwa mwezi Julai 2024, ni asilimia 1.5, uwiano huu umepungua kutoka asilimia 4.4 kwa mwezi Julai 2023, na kwa asilimia 3.5 kwa mwezi Juni, 2024," alisema.

Faki alisema bidhaa zilizosafirishwa kwa mwezi Julai zilikuwa na thamani ya Sh. bilioni 2.5, ambayo imepungua kwa asilimia 71.6, ikilinganishwa na mwezi Julai, 2023 na kwa asilimia 52.8 kulinganishwa na Juni 2024.

Alisema kundi la vyakula na wanyama hai liliongoza kwa kuchangia asilimia 65.5 ya thamani yote ya usafirishaji bidhaa.

Faki alizitaja bidhaa zilizosafirishwa ni pamoja na chumvi, vinywaji baridi na pumba.

Alisema usafirishaji bidhaa kwa nchi tano zilizoongoza kwa mwezi Julai, ulifikia asilimia 75.3 ya thamani ya bidhaa zote zilizosafirishwa, ambapo China iliongoza kwa bidhaa zilizofikia thamani ya Sh. milioni 619.1, sawa na asilimia 30.1.

Kuhusu takwimu za uagizaji bidhaa, alisema zilikuwa na thamani ya Sh. bilioni 141.1, zikiwa zimepungua kwa asilimia 13.4 kulinganishwa na mwezi Julai 2023, lakini zimeongezeka kwa asilimia 13.6 kulinganisha na mwezi Juni 2024.

Faki alisema kundi la mashine na vifaa vya usafirishaji lilichangia asilimia 44.4 ya bidhaa zote zilizoagizwa.

"Bado hali inaonesha kuwa vizuri kiuchumi na kuleta faraja kwa wananchi na taifa kwa ujumla," alisema Faki.

Mchumi Mkufunzi Mwandamizi Skuli ya Biashara, Dk. Estella Ngoma Hassan alisema ipo haja ya kuongezwa thamani bidhaa zinazosafirishwa nje ili kuongeza mapato ya fedha za kigeni.



**ABBY**
UKURASA 13





# Marco alipata tatizo hatari la moyo

IMEELEZWA tatizo la moyo alilopata mwimbaji wa Injili, Marco Joseph wa kundi la Zabron Singers, lilikuwa kubwa na upasuaji wake unakuwa mgumu na hatari.

Kulingana na Profesa Harry Magori, ambaye pia ni mjomba wa Marco, amesema ndugu yake alipata tatizo katika mrija mkubwa wa moyo wa kusafirisha damu mwilini na alihitaji upasuaji wa haraka ili kuokoa maisha yake.

Marco alifariki dunia juzi wakati akipatiwa matibabu katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Profesa Magori, ambaye ni tabibu mbobezi wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, ameeleza kwamba tatizo hilo huwapata sana watu wenye umri wa kuanzia miaka 50 na kuendelea na wale wanaovuta sigara.

"Marco hakuwa anavuta sigara lakini alipata tatizo hilo, alipokuja JKCI alitakiwa kufanyiwa upasuaji mkubwa wa kufungua kifua ili kubadilisha mshipa mkubwa wa moyo," amesema Profesa Magori.

Amesema kitaalamu upasuaji wa aina hiyo humpa mgonjwa asilimia 50 ya kupona au kupoteza maisha kutokana na kupoteza damu nyingi.

"Madaktari walifanikiwa kumfanyia upasuaji salama na kumrudisha katika wodi maalum, lakini muda mfupi alipoteza maisha baada ya kupata presha ya kushuka," ameongeza.

BASI SAWA

## Baba Levo asumbuliwa na wivu



MSANII wa muziki Baba Levo, amesema kila anapoingia sehemu chawa wote wanamkimbia kutokana na yeye kuwa maarufu zaidi.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, msanii huyo mcheshi amesema anakwenda Zanzibar kushiriki tamasha la Kizimkazi, lakini huko atawatimua chawa wote wanaong'angania kuwa karibu na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Nikifika mahali nashangaa chawa wote wananikimbia, sasa nawaambia nakuja Kizimkazi kuwaondoa Mwijaku na Doto Magari," amesema.

## Hapa ni Ali Kiba kule Jay Melody



MASHABIKI wa muziki wa Bongo Fleva, wanatarajia kusikia wimbo mpya utakaowashirikisha wasanii maarufu Ali Kiba na Jay Melody.

Baada ya kuona video ya wanamuziki hao wakiwa studio, wafuasi wao walivamia mitandao ya kijamii na kuwataka wanamuziki hao kuachia haraka kolabo hiyo ambayo wanatarajia kuwa kali.

Jay Melody na Ali Kiba itakuwa mara ya pili kufanya kazi pamoja na pengine ndiye wasanii pekee nchini wanaopiga muziki wao bila kubadilika.



## ANJELLA KAHEMEWA NA ZUCHU

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Anjella, amesema Mungu pekee anajua kile alichotendewa na Zuchu kwa kumnunulia gari jipya.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa gari hilo aina ya Subaru, Anjella amesema mpaka sasa haamini kile kinachoendelea katika maisha yake, hivyo anamshukuru Zuchu kwa kumpatia tena furaha.

"Sikuwa na ukaribu sana na Zuchu, sikuwa na mazoea naye nakumbuka tulikuwa tunachati mara moja moja, aliponiambia ataninunulia gari hata kesho, nilishangaa na sikuamini kabisa, lakini imekuwa kweli," amesema Anjella.



## Abby afurahia mabadiliko

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Abby Cham, amesema amefurahi kuona wanawake wameanza kujitokeza kwa wingi katika tasnia ya burudani.

Amesema pamoja na kuwa na mapungufu mengi katika sekta ya Sanaa, lakini imepiga hatua kutokana na mabadiliko yanayojitokeza ikiwamo kuwaunga mkono wasanii wa kike.

"Wasanii wa kike sasa wametawala sehemu kubwa katika tasnia ya muziki kuliko zamani, kuna waimbaji, maDj na hata waandishi wa nyimbo. Hili ni jambo la kujivunia," amesema Abby Cham.

FILAMU

# Mke haokotwi, anatafutwa

**Na Adam Fungamwango**

KUNA msemo unaosema kosea vitu vyote duniani, lakini usikosee kuoa au kuolewa. Msemo huu una maana kuwa ukikosea kumpata mwenza, basi utakuwa na matatizo makubwa kwenye maisha yako. Ni kwa sababu mke au mume ni mtu wa karibu mno ambaye unaishi naye kila siku na mko naye muda mrefu mno kuliko ndugu zako.

Binadamu akishakuwa mtu mzima huacha kuishi na ndugu zake na kuanza kuishi ni mtu mwingine kabisa ambaye naye ametoka kwingine. Inafaa umpate mtu ambaye utaishi naye kwa hali ya upendo, furaha na amani, lakini ikiwa kinyume chake ni mateso makubwa.

Ndiyo maana tunafundishwa kuwa makini mno kwenye kuchagua mke au kumfahamu vizuri mwanaume unayekwenda kuishi naye. Hii imeonekana kwenye filamu ya 'I think i hate my wife', aliyekutana na mwanamke tu barabarani bila kumfahamu vizuri, baadaye akamgeuza kuwa mkewe, alivyopata tabu na mateso.

Imechezwa na Simom Mwapagatwa maarufu kama 'Rado', Jacob Steven 'JB', Shamsa Ford, na wengineo.

Rado akiwa ndani ya gari yake, akakutana na msichana anayeonekana anahitaji msaada wa lifti, lakini pia anaonekana si mwenyeji wa jiji la Dar.

Anampeleka nyumbani kwake. Awali alionekana kumsaidia kama mfanyakazi wa ndani, lakini kadri siku zilivyozidi kusonga mbele, ndipo alipouona uzuri wa msichana huyo.

Akaamua kumuoa awe mkewe. Usilolijua ni kama usiku wa kiza, kumbe mwanamke yule ni mtoto wa mjini aliyekuwa akifanya kazi kwenye majumba ya starehe jijini.


Pia mwanamke huyo alikuwa na mambo ya kishirikina. Alimtengeneza Rado hakufurukuta. Akawa sasa anafanya kila anachoambiwa na mkewe Shamsa.

Mamilioni ya pesa yanahamishwa kwenye akaunti yake na siku chache baadaye, watu wanavamia nyumbani kwake, wakitaka atoe hati ya nyumba.

Kumbe yale yote yako nyuma ya mkewe Shamsa. Mikasa iliyompata, ilimfanya Rado awe kichaa. JB ambaye alikuwa rafiki yake na alikuwa akifanya naye kazi, alimtafuta na alipompata akamhamishia nyumbani kwake, huku akimuuguza. Akapona, lakini akaanza na moja. Rado akawa kwenye mahusiano mengine na mpwa wa rafiki yake JB kwa sababu ndiye aliyekuwa naye karibu akimfariji.

Wakaanzisha biashara, ambayo ilianza kuwa kubwa na kujipatia faida, mwisho wakaamua kuoana.

Rado, mkewe mpya, JB na mkewe waliamua kwenda kwa Mchungaji kwa sababu Shamsa alionekana bado anawafuatilia kwa nguvu za kishirikina. Mchungaji anavunja nguvu za kishetani, Rado anaanza maisha mapya na mke mwingine.




## WABONGO WANAOMUIGA FRANCO

**Na Adam Fungamwango**

WALA siyo siri kuwa muziki wa zamani Tanzania ulitawaliwa au kuathiriwa zaidi na staili ya upigaji kutoka Zaire (sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo) na Congo Brazaville.

Kulikuwa na msururu wa bendi nyingi sana kwenye nchi hizo mbili na wanamuziki bora kabisa, kiasi cha bendi nyingi nchini kuiga nyimbo kwa mirindimo, huku wakibadilisha tu maneno.

Mfano wa hilo ni wimbo wa Kilwa Jazz, 'Napenda Nipate Lau Nafasi', ambao ni maarufu hadi leo.

Huu wimbo ni kama kopi tu ya wimbo wa 'Mokolo Nakukufa' ulioimbwa Tabu Ley Rochereau mwaka 1966.

Ni maneno yaliyobadilika pamoja na lugha, lakini jinsi unavyoimbwa na upigaji unafanana kabisa.

Huo ni mfano tu, zipo nyimbo nyingi sana kama hizo za Congo zilizobadlishwa na kuimbwa kwa lugha ya kishwahili na bendi za Tanzania miaka hiyo.

Ukiacha hilo kuna aina ya upigaji. Kwenye ala ya magita ongozi ya solo yaligawanyika sehemu mbili.

Upigaji wa kwanza uliitwa soukous wa pili uliitwa odemba.

Leo nitauzungumzia mtindo wa odemba. Ni staili iliyobuniwa na mfalme wa rhumba duniani, Luambo Luanzo Makiadi Franco.

Odemba ni staili moja ya rhumba yenye upigaji wa gita kwa mtindo wa kente.

Ni staili ambayo gita linapigwa kwa nyuzi mbili mbili kwa mpigo. Wakati mwingine mpigaji anafunga kifaa mfano ya pingu hivi katikati au mbele kwenye mpini na nyuzi za gita.

Sasa hapo mpigaji alipiga, sauti yake inakuwa kama anapiga chuma hivi, kwa sababu nyuzi zinakuwa zimekaza sana, huku zikipigwa dabo.

Sikiliza nyimbo nyingi za Franco jinsi gita lake linavyolia, kama kwamba mtu anagonga na si nyuzi.

Hapa Tanzania kuna wanamuziki wengi waliiga aina ya upigaji huo wa staili ya kente au mwenyewe aliita odemba.

### Mbaraka Mwinshehe Mwaruka

Huyu si upigaji tu, kwani alimuiga Franco kwa kila kitu hadi kufuga ndevu. Na hata wajihi wao walifanana sana. Ukimuoa Mbaraka alikuwa amefanana sana na Franco.

Tukija kwenye muziki, wote wawili wanapiga magita ongozi ya solo na kuimba pia.

Hayati Mbaraka alimuiga Franco kwenye upigaji aina ya kente. Ukitaka kumsikia vizuri, sikiliza wimbo wa 'Benki ya Taifa ya Biashara' na 'Unanitafutia nini?'. Humo kuna kente la kufa mtu.

### Said Mabera

Marehemu Said Mabera, aliyekuwa kiongozi wa bendi ya Msondo Ngoma Music, tangu wakati inaitwa Juwata Jazz.

Huyu nyimbo zake zote amepiga kwa staili hiyo ambayo Franco amekuwa akiipiga.

Lakini ukitaka kujua shughuli yake sikiliza vibao kama 'Faulata', 'Piga Ua Talaka Utatoa', 'Kalumanzira', na 'Ajali'. Unaweza ukazani kama anayepiga ni Franco mwenyewe.

### Shem Karenga

Alikuwa ni kiongozi wa bendi ya Tabora Jazz wana Segere Matata. Marehemu Shem, naye alikuwa ni mtaalam wa upigaji wa gitaa la staili ya kente. Linasikika zaidi kwenye nyimbo kama 'Sarafina', 'Dada Asha', 'Dada Remmy', 'Halima', 'Chakula Kwa Jirani', na 'Farida'.

### Hamza Kalala

Huyu naye ni mfuasi wa Franco. Karibuni nyimbo zake zote anapiga kwa mtindo wa odemba.

Msikilize kwenye nyimbo nyingi za Vijana Jazz, kama vile 'Amba', 'Madaraka kwenye Baa', 'Stella', 'Tambiko la Pambamoto', 'Bujumbura' na nyingine nyingi alizopiga kwa mtindo huo.

### Shaaban Yohana 'Wanted'

Huwezi kuwataja wafuasi wa Franco hapa Bongo kama hujamtaja marehemu Shaaban Yohana 'Wanted.' Ni hatari kabisa. Msikie kwenye nyimbo za Vijana Jazz kama 'Heshima ya Mtu', 'Aza Umeniumbua' na nyingine nyingi.




# Krane amkunjia roho Davido

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Dammy Krane, amedai kuwa msanii mwenzake Davido alitoa pesa ili ashtakiwe kesi ya uwongo ya utakatishaji fedha.

Akitumia ukurasa wake wa X, Krane, amemtuhumu Davido kuwa atawajibika ikiwa kitamtokea chochote kwa sababu anamtafuta kwa ubaya.

"Iwapo chochote kitatokea kwangu Davido anapaswa kuwajibika, amewalipa polisi ili kunikamata na kuandika mashtaka ya uwongo kwamba ninatakatisha fedha," amesema Krane.



## Lopez,Affleck talaka hiyoo..

HATIMAYE Mwimbaji na mwigizaji wa Marekani, Jennifer Lopez amewasilisha rasmi maombi ya talaka dhidi ya mume wake, Ben Affleck.

Kwa mujibu wa TMZ, Lopez aliwasilisha kesi ya kuvunjwa kwa ndoa yao ambayo imedumu kwa miaka miwili katika mahakama ya Los Angeles.

Mgogoro huo ambao awali ulikuwa kama uvumi, uliwekwa wazi kufuatia ombi hilo la talaka baada ya wawili hao kujulikana wanaishi katika nyumba tofauti na kufuatia tukio la kuuzwa kwa nyumba yao waliyonunua pamoja.

## Ugomvi wa ndugu, hauna hakimu

MGOGORO unaoendelea kati ya wanamuziki wawili ambao ni mapacha, Paul na Piter Okoye, umemfanya kaka yao Jude kuingilia kati na kuwataka ndugu hao kuwa wamoja.

Wanamuziki hao wa kundi la P-square, wamekuwa wakishtumiana vikali kuhusu kuharibiana kikazi na matumizi mabaya ya pesa zilizotokana na kazi zao.

Rudeboy, amewaambia wadogo zake kuwa hata kama hawako katika kundi moja, lakini wana wajibu wa kujumuika pamoja kama ndugu.

"Hata tusipofanya kazi Psquare, bado hatuwezi kuwa ndugu? Hata tusipofanya muziki, hatuwezi kuwa ndugu? Ni lazima wakae pamoja kama ndugu wa kuzaliwa," amesema.





## Mwacheni marehemu apumzike

MJANE mwa mwanamuziki Afro Beat kutoka Nigeria, marehemu Mohbad, amewaomba mashabiki waepuke kumsema vibaya mume wake.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Wunmi ameandika ujumbe mrefu kwa wafuasi wao ambao wanaendeleza mabishano kuhusu kifo cha Mohbad, ambacho kina utata.

"Kama wengi wenu mnavyojua, nimevumilia shutuma nyingi za kudharauliwa na za uwongo kutoka pande mbalimbali familia, marafiki na hata wageni.

"Pamoja na uchungu, nimechagua kukubaliana na hali hii mbaya kuwa sehemu ya safari yangu, nataka niweke wazi kuwa sitajihusisha na mijadala ya hadhara au kujaribu kukabiliana na uongo unaoenezwa juu yangu, kutetea ukweli wangu mahakamani, sio kwenye mitandao ya kijamii, hata hivyo, lazima nizungumze kwa niaba ya Ilerioluwa, ambaye hayupo tena kujitetea," amesema.

## Oprah amkubali Kamala

MTANGAZAJI wa televisheni Oprah Winfrey, ameungana na mastaa wengi kumuunga mkono Kamala Harris katika mbio zake za kuwania urais wa Marekani.

Oprah alijumuika na wanachama wengine wa Democratic katika mkutano mkuu na kueleza kwamba wamarekani sasa kuchagua busara badala ya upuuzi.

"Tuchague ukweli, tuchague heshima, tuchague furaha "Kwa sababu hiyo ndiyo Marekani bora zaidi." Oprah aliwaambia umati wa watu waliokuwa wakimsikiliza.

Kumuunga mkono Harris kumesaidia kukipa nguvu zaidi chama cha Democtrats ambacho wiki hii kimeshuhudia wasanii mbalimbali wakijitokeza kujiunga nacho.



## Wafanyabiashara watishia kutunza fedha katika chaga

**Na Oscar Assenga,** TANGA

JUMUIYA ya Wafanyabiashara Tanzania (JWT) mkoani Tanga imesema haitaki akaunti za wafanyabiashara zishikiliwe na Mamlaka ya Mapato (TRA) na iwapo hali hiyo ikiendelea, watarudi katika utaratibu wa zamani wa utunzaji fedha katika chaga.

Katibu wa Jumuiya hiyo Mkoa wa Tanga, Ismail Masoud aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wa NMB Business Club 2024 uliofanyika jijini hapa.

Alisema ukamataji huo ukiendelea watalazimika kufanya hivyo kwa sababu hawataki kuona vitendo hivyo vikiendelea.

Masoud alisema akaunti ya benki ni siri ya mtu na benki na wanataka mfumo wa kutumia fedha taslimu uachwe, watumie kuchanja.

"Niwaambie benki ndio zinafanya kazi sana kuliko mitandao, lakini Tanzania mitandao ndio inafanya kazi zaidi kuliko benki na mifumo ya fedha Tanzania, unazunguka sana katika mifumo ya mitandao kuliko benki.

"Inabidi tushirikiane na jumuiya za wafanyabiashara tuone namna ya kufanya mifumo ya fedha ipitie katika benki. Lakini wengine hawalipi kodi, hilo ni tatizo, linawaumiza wafanyabiashara.

"Hivyo, NMB lazima tubadilishe sera, asilimia 60 ya wafanyabiashara nchini ni machinga, hawalipi kodi, asilimia 40 ni wafanyabiashara wanaolipa kodi na kuchukua mikopo kwao.

"Kuna namna mbili wanatakiwa kufanya biashara walipe kodi na wanatakiwa kufanya biashara kurudisha mikopo, hivyo mifumo ya benki lazima ibadilike kulingana na hali ya biashara ilivyo," alisema.

Alisema wasipobadilisha sera, hali ya biashara itaendelea kuwa ngumu, huku akitaka kuwapo utaratibu mzuri wa benki kudai madeni ya wafanyabiashara waliokopa.

Pia alisema kuna haja kuunda kamati za kufuatilia kila wilaya ambazo zitakuwa mwarobaini wa kuondokana na tatizo la kuuza nyumba zao na mali ili kufidia mikopo hiyo pale wanaposhindwa kulipa.

Aliwataka wafanyabiashara wasiuziwe nyumba zao na mali zao wanazomiliki, bali iundwe kamati ya madeni kila wilaya itakayowezesha upatikanaji fedha zinazodaiwa.

Meneja wa NMB Kanda ya Kaskazini, Baraka Ladislaus, alisema lengo la kuanzishwa NMB Business ni kuwafanya wawe karibu na wateja.

Alisema kupitia huko wanapata fursa ya kusikia changamotoo mbalimbali za wateja wao na hivyo kuwasaidia kufanya maboresho katika huduma ambazo wamekuwa wanazitoa.

# Utapiamlo mkali waua 13, ma-DED kitanzini

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, amesikitishwa na vifo vya watoto 13 waliopoteza maisha kutokana na utapiamlo mkali mkoani mwake.

Kutokana na vifo hivyo, kiongozi huyo ametishia kushtaki kwa Rais Samia Suluhu Hassan wakurugenzi wote wa halmashauri kwa kushindwa kutenga fedha za lishe kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Alisema atafanya hivyo kupitia kikao cha lishe cha kitaifa kitakachofanyika Agosti 30 mwaka huu, ambacho kinatarajiwa kuongozwa na Rais Samia.

Watoto waliobainika kupata utapiamlo mkali na waliopoteza maisha kwa Halmashauri ya Simanjiro, waligundulika watoto 102 na vifo vitano.

Maeneo mengine ni Kiteto walikogundulika 52 (vifo vitano), Hanang' wamegundulika 50 (vifo viwili) na Halmashauri ya Mji wa Babati walikogundulika 15 na kifo kimoja, huku Halmashauri ya Wilaya ya Babati ikibainika kuwa na watoto 141 ambao wote walitibiwa na hakuna kifo.

"Katika mikoa ambayo nimeongoza, Manyara ndio wakurugenzi wake wagumu kutenga fedha za lishe kwa watoto chini ya miaka mitano," alisema Queen.

Alisema kuwa katika kikao cha kitaifa, hatawaficha siri - kwamba ionekane wanatenga fedha za lishe kwa kila mtoto chini ya miaka mitano Sh. 1,000 ilhali hawafanyi hivyo.

Queen alitumia fursa hiyo kumwagiza Katibu Tawala wa Mkoa huo, Maryam Muhaji, kuwaandikia barua wakurugenzi wote kwamba, hawakutenga fedha hizo na wapatiwe kuzitia saini na kumkabidhi, ili kumpatia Rais ambaye ndio aliwapa kazi.

Alisema suala hilo ni la kitaifa na wakuu wa mikoa ndio wanatia saini mikataba ya lishe na wao kuwasainisha wakuu wa wilaya ili waisimamie.

"Kwa picha hii, wakuu wa wilaya hamsimamii mikataba ya lishe, mko 'bize' kusimamia miradi ya madarasa ili aje kusomea nani?" Mkuu wa Mkoa alihoji.

Ofisa Lishe wa Mkoa wa Manyara, January Dalushi, alisema hali ya lishe kimkoa inaendelea kuimarika kwa mujibu wa taarifa ya Utafiti wa Tanzania Demographic Health Survey (TDHS) wa mwaka 2022.

Alisema ripoti ya utafiti huo inaonesha kuwa mkoa una asilimia 32 ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano waliodumaa.

Dalushi alisema kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai mwaka jana hadi Juni 30 mwaka huu, watoto 442 wenye umri chini ya miaka mitano, walibainika kuwa na utapiamlo mkali na watoto 435 sawa na asilimia 98.4 walipona huku watoto 13 wakipoteza maisha.

Akizungumza na Nipashe jana, mkazi wa Babati, Adrian Malle, alisema ili kudhibiti utapiamlo mkali katika jamii, ni lazima wataalamu wa lishe na afya waingie mitaani kutoa elimu kwa wananchi namna ya kuwa na ulaji bora kwa watoto.



Diwani wa kata ya Kicheba, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Hamisi Mkodingo akisoma taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2021-2024, wakati wa kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM ya kata hiyo, mapema wiki hii. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# DC aonya viongozi kulegalega usimamizi ukusanyaji mapato

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Wilaya Moshi, Kamishna Jenerali mstaafu James Kaji ametoa onyo kwa viongozi watakaoonesha kulegalega katika usimamizi wa mapato na uharibifu wa mazingira.

Pia ameitaka manispaa hiyo kushirikiana na Mamlaka ya Mapato (TRA) kuhakikisha ushuru wa huduma unakusanywa; kama kuna changamoto wafike ofisini kwake kujadiliana.

Alielekeza hayo jana, akisema kuwa licha ya Moshi kuonekana kuwa na maendeleo, kuna shule zinakabiliwa na uhaba wa matundu ya vyoo na uchakavu wa miundombinu.

"Niombe ushirikiano kwa viongozi wote, hasa Baraza la Madiwani. Mimi ni mtu mwema ingawa nina sura mbili; ya malaika tukifanya vizuri na ya ibilisi tukienda tofauti.

"Ninaamini kabisa tutakuwa katika sura ya malaika. Hali ninayoona Moshi hakuna tatizo, bali ni kuhamasisha utekelezaji," alisema.

Akitoa taarifa ya maendeleo ya mwaka 2023/24, Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi, Mwajuma Nasombe, alisema kuwa kwa mwaka 2023/24, halmashauri ilikadiria kupokea makusanyo ya mapato ya Sh. bilioni 51.3, lakini hadi kufikia mwisho wa mwaka, walipokea Sh. bilioni 49.3 sawa na asilimia 95.

"Kwa makusanyo ya ndani, manispaa ilikadiria kukusanya Sh. bilioni 8.8. Hadi mwezi Juni 2024, manispaa ilikusanya Sh. bilioni 8.9 sawa na asilimia 101," alisema.

Meya wa Manispaa hiyo, Zuberi Kidumo, alisema jitihada mbalimbali za wataalamu zilisaidia kuvuka malengo, hivyo kuwaomba kuziongeza ili kuhakikisha wananchi wanapata maendeleo.

"Tutaendelea kufanya kazi kwa bidii kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo. Sisi ni wasimamizi tu ila ninawaomba wananchi wote wajitahidi kutimiza wajibu wao, hasa ulipaji kodi mbalimbali," alisema Kidumo.

MAKALA

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Makosa 30 ambayo watoto wa zamani walikuwa wakila bakora



**Na Adam Fungamwango**

WATOTO wa zamani walikuwa wakiishi na wazazi au walezi wao kama wapo jeshini hivi.

Siku hizi kuna kama hali ya kudekezwa fulani hivi kwa watoto, na hiki ndicho kinachotajwa kuwa ni kuporomoka kwa heshima, utamaduni na maadili.

Watoto wa sasa wanatajwa kuwa na ukosefu wa adabu kwa wakubwa, na sababu kubwa ni kwamba hawafundishwi kuheshimu watu waliowazidi umri.

Wala si ajabu tena sasa hivi kukuta kijana tu mwenye umri wa miaka 20 hadi 25 akiwa ameketi raha mustarehe kwenye siti ya daladala huku mtu mzima wa miaka 60 au zaidi akiwa amesimama kando yake. Hana hata habari, wakati mwingine anachukua na simu yake ya mkononi anachati ili ionekane kwamba hajamuona.

Wakati mwingine mama mtu mzima na miguu imevimba, lakini kijana mwenye nguvu zake amekaa kwenye siti kana kwamba gari hilo linasafiri kwa siku mbili, hivyo hawezi kusimama.

Huo ni mfano mdogo tu unaoonekana kwa haraka unaoashiria kuwepo kwa mmomonyoko wa maadili ambapo kwenye miaka ya 1990 kurudi nyumba usingeweza kuukuta.

Nilishawahi kusema kuwa wazazi wa zamani walikuwa kama wamesoma shule moja ya uleaji watoto. Wote walikuwa wana nia moja tu, ukienda kwa baba na mama huyu, ukirudi kwa baba wa rafiki yako, au kwenu, utakuta ni vile vile, hakuna unafuu.

Yote hayo wazazi walikuwa wakiwafunza watoto wao jinsi gani ya kuwa na adabu, heshima,kwani walijua hawatoweza kuishi nao milele. Kuna siku wataondoka kwenye mikono yao na kwenda kuishi sehemu nyingine. Pia walikuwa kuna siku ambayo wao hawatokuwepo duniani, hivyo watoto wao wasije kuwa mzigo au kudhararika.

Waliwafundisha watoto uvumilivu, na hii imewafanya kuishi kwa kutegemea nguvu zao kufanya kazi, na siyo 'uchawa', au kutaka kupata maisha mazuri kirahisi na kwa njia ya mkato. Ndiyo maana kuna wakati watoto wa zamani walionekana kama wanaishi kwenye kambi za jeshi kutokana na adhabu walizokuwa wanapata kwa wazazi wao.

Wazee wa zamani waliwafundisha watoto wao namna ya kujitegemea, unaweza kumpatia mtoto koleo, ili kuzibua maji ya mvua yaliyotuama, badala ya kumwita kijana mtaani kwa malipo kama wanavyofanya wa sasa.

Leo tunawaletea makosa 30 ambayo wazee wa zamani walikuwa wakitembeza bakora kwa watoto.

Kwanza kabisa, usiposalimia wakubwa asubuhi unapigwa na usiposalimia wageni unapigwa.

Ukinawa wakati wa kula kabla ya wageni unapigwa, ukilia bila sababu unapigwa, ukinyanyuka wakati wa kula kabla ya wakubwa kuinuka unapigwa, wakubwa wakiwa wamekaa wewe ukaenda kusimana pembeni unapigwa, ukikaa wakubwa wamesimama unapigwa.

Ukitumwa dukani ukachelewa kurudi unapigwa, ukichelewa kurudi toka shuleni unapigwa, ukiwahi kurudi shuleni vile vile unapigwa. Ukililia wageni wakati wanaondoka, wakitoka unapigwa, kujipitisha pitisha wageni wakiwa wanakula unapigwa, kujibu ovyo wakubwa unapigwa, kutukana watu wazima, watoto au rika lako unapigwa, ukiwa mbishi bila sababu unapigwa, ukipigwa ukilia unapigwa ili unyamaze, ukipigwa umenyamaza unapigwa ili ulie.

Makosa mengine ni kwamba, ukipigwa shuleni ukaenda kusema nyumbani, unapigwa, ukianza kula nyama kabla ya wakubwa unapigwa, ukila kwa jirani ukibainika unapigwa, ukinawa kabla ya wageni unapigwa. Pia, ukianza kunawisha watoto badala ya wakubwa unapigwa, ukianza kunawisha wenyeji badala ya wageni mkimaliza kula unaitwa chumbani unapigwa, ukimkuta mtu mzima na hujampokea unapigwa, ukienda kusema kama umepigwa, unapigwa.

Kama vile haitoshi, mtu mzima akipita kama mnacheza hamjamshughulikia au kumsalimu mnapigwa, ukienda nyumba za watu, ukaona kitu au ukasikia habari yoyote ukaileta nyumbani unapigwa, ukipewa hela na mtu asiyefahamika au hata anayejulikana unapigwa.

Fauka ya hayo, ukichagua chakula au mboga unapigwa, ukiongea wakati wa kula unapigwa, ukiwa na marafiki wasioleweka makwao unapigwa, na Mtu mkubwa akija kukuchongea nyumbani hata kama jambo lenyewe si la kweli unapigwa.

Haya ndo makosa ninayokumbuka, ndugu msomaji kama kuna mengine unayoyakumbuka tuandikie.

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

# Kamala amuita Trump, mbabe anayependelea

**CHICAGO,** MAREKANI

MAKAMU ra Rais wa Marekani, Kamala Harris amekubali rasmi uteuzi wa kuwa mgombea wa urais wa chama cha Democrat katika kongamano la kitaifa la chama hicho lililomalizika juzi.

Wakati akitoa hotuba ya kukubali uteuzi huo, Harris aliahidi kuongoza kwa ajili ya Wamarekani wote.

Mgombea huyo alizungumzia masuala mbalimbali ya atakayoyashughulikia ikiwamo usalama wa mpaka, ambalo Donald Trump mgombea wa Republican amekuwa akitumia kumshambulia kila mara.

Akizungumzia kuhusu hatma ya Marekani, Harris alisema anaipenda nchi yake kwa moyo wote na analiona taifa ambalo liko tayari kusonga mbele.

"Ninaipenda nchi yetu kwa moyo wangu wote. Popote ninapoenda na kila mtu ninayekutana naye, naona taifa ambalo liko tayari kusonga mbele, tayari kwa hatua inayofuata na safari ya ajabu ya Marekani," alisema huku akishangiliwa na wanachama wa Democrat.

Alisema Wamarekani wana mengi zaidi ya kuwaweka sawa kuliko yale yanayowagawanya.

"Hakuna hata mmoja wetu anayepaswa kushindwa ili sisi sote tufanikiwe," alisema.

Harris alisema anatofautiana na timu ya kampeni ya Trump, ambaye anasema yuko akiidhalilisha Marekani.

Mgombea huyo pia alizungumzia kuhusu muswada wa usalama wa mpaka wa pande mbili ambao ulisambaratika katika Bunge la Congress mwaka huu baada ya Trump kuwataka wabunge wa Republican kupiga kura ya kuukataa.

"Donald Trump anaamini kuwa makubaliano ya mpaka yataathiri kampeni yake, kwa hivyo aliamuru washirika wake ndani ya Congress kuua mpango huo," aliongeza Harris. Harris alisisitiza kuwa anapanga kurudisha muswada huo na kuutia saini kuwa sheria.Idadi kubwa ya wahamiaji walizuiliwa kwenye mpaka wakati wa utawala wa Trump, lakini idadi ya vivuko vya wahamiaji visivyo halali sasa imepungua kwa miezi mitano mfululizo.

Mgombea huyo alisema kuwa nchi zinazoongozwa na watawala wa kimabavu zinampigia debe Trump kwa sababu wanaamini ni rahisi kudhibiti kwa maneno ya kubembeleza na kupendelea.

"Wanajua Trump hatawajibisha watawala kwa sababu anataka kuwa mbabe mwenyewe," aliambia umati wa watu waliokuwa wakishangilia.

Wakati huo huo, viongozi wa chama cha Democrat, walikataa matakwa ya waandamanaji ambao walishinikiza kumruhusu Mpalestina kuzungumza katika mkutano mkuu wa chama hicho.

Wajumbe wa chama hicho ambao wanapinga uungaji mkono wa Marekani wa vita vinavyoendeshwa na Israel katika Ukanda wa Gaza, waliweka mgomo wa kukaa nje ya milango ya uwanja siku ya kumaliza mkutano huo.

Hadi kufikia saa 12 jioni waandamanaji walikuwa na matumaini kusikia jibu kutoka kwa timu ya kampeni ya Kamala Harris, kukubali ombi hilo. **BBC**



Mgombea wa Urais kupitia chama cha Democrat, Kamala Harris, akiwapungia mkono wanachama wa chama chake katika mkutano mkuu uliofanyika Chicago nchini Marekani. **PICHA: REUTERS**

# Polisi Kenya yatoa donge nono atakayetoa taarifa ya muuaji

**NAIROBI,** KENYA

JESHI la Polisi nchini Kenya limetangaza zawadi ya pesa taslimu kwa mtu yeyote atakayetoa taarifa za kuaminika zitakazowezesha kukamatwa kwa mshukiwa wa mauaji ya wanawake jijini Nairobi.

Mtuhumiwa huyo Collins Jumaisi, ambaye anahusishwa na kuua, kukatakata viungo, kufunga miili ya watu kwenye magunia na kisha kuitupa dampo la takataka, alitoroka mahabusu ya polisi na kwenda sehemu isiyojulikana.

Hata hivyo, idara ya upelelezi (DCI) haikutaja kiwango cha pesa zitakazotolewa.

Polisi ilianzisha msako kuanzia Jumanne baada ya Jumaisi, kutoroka kutoka kituo cha polisi cha Gigiri pamoja na raia 12 wa Eritrea.

Kutokana na tukio hilo, askari watano waliofikishwa mahakamani juzi kwa kushukiwa kumsaidia mshtakiwa kutoroka.

Washtakiwa wote wameachiliwa kwa dhamana, licha ya waendesha mashtaka kutaka waendelee kukaa rumande kwa siku 14.

Wakati huo huo, Wizara ya Afya ya Kenya, mwanamume dereva wa lori mwenye historia ya kusafiri kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (D.R.C.) amepatikana na virusi vya Homa ya Nyani au Mpox.

Dereva huyo alifanyiwa uchunguzi katika mji wa mpakani wa Busia magharibi mwa Kenya.

Sampuli yake ilithibitishwa kuwa na virusi katika uchunguzi wa maabara.

Mtu huyo ametengwa na yuko chini ya uangalizi wa karibu.

Aidha uchunguzi wa kina wa watu wanaoshukiwa kuwa na virusi vya Mpox umeimarishwa katika eneo hilo na katika kaunti zote ili kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huo.

**DW**

# Botswana yagundua jiwe kubwa la almasi mgodini

**GABORONE,** BOTSWANA

BOTSWANA imesema imepata moja ya almasi kubwa kuwahi kuchimbuliwa katika migodi yake.

Kampuni ya uchimbaji madini ya Canada ya Lucara Diamond Corp, ilisema katika taarifa yake iliyotolewa juzi kuwa almasi hiyo iliyotajwa ya kipekee kutoka kwenye mgodi wake wa Karowe, uliopo magharibi mwa nchi hiyo.

Lucara alisema lilikuwa jiwe lenye ubora wa juu na lilipatikana likiwa katika hali nzuri kwa kutumia teknolojia ya X-Ray.

Uzito huo unaifanya kuwa almasi kubwa zaidi kupatikana katika zaidi ya miaka 100 na ya pili kwa ukubwa kuwahi kuchimbwa mgodini baada ya Almasi ya Cullinan iliyogunduliwa Afrika Kusini 1905.

Cullinan ilikuwa na karati 3,106 na ilikatwa kuwa vito, ambavyo baadhi ni sehemu ya vito vya taji ya Mfalme wa Uingereza.

Almasi kubwa nyeusi iligunduliwa nchini Brazili mwishoni mwa miaka ya 1800, lakini ilipatikana juu ya uso na iliaminika kuwa sehemu ya miamba ya angani ambayo huanguka duniani.

Botswana ni nchi ya pili kwa uzalishaji wa almasi na imechimbua mawe yote makubwa zaidi duniani katika miaka ya hivi karibuni.

Kabla ya ugunduzi huu, almasi ya Sewelo, ambayo ilipatikana katika mgodi wa Karowe mnamo 2019, ilitambuliwa kama almasi ya pili kwa kuchimbwa kwa ukubwa duniani kwa kuwa na karati 1,758.

**TRT**

# HABARI PICHANI



Msururu mkubwa wa abiria wakisubiri usafiri wa mabasi ya mwendokasi, katika kituo cha daladala Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mtondo, Kata ya Nambilanje, wilayani Ruangwa, mkoa wa Lindi, juzi. **PICHA: OWM**



Mfanyabiashara Mkurugenzi wa Hotel ya Regail Naivera, Primus Msele akichangia mada, wakati wa mkutano wa Klabu ya Biashara ya NMB, ulioshirikisha wafanyabiashara mbalimbali, jijini Tanga juzi. **PICHA: OSCAR ASSENGA**



Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga (katikati), akizungumza wakati akifungua semina ya usambazaji wa matokeo ya utafiti wa afya na mtoto na viashiria vya malaria kwa mwaka 2022 inayowashirikisha wataalam wa afya kutoka mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara, mkoani humo hivi karibuni. Wengine ni Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Victorina Ludovick (kushoto), Meneja Takwimu Mkoa huo, Naing'oya Kipuyo (kulia) na Mratibu wa Utafiti, Elinzuu Nicodemo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene akizungumza na waamini wa Kanisa Katoliki Jimbo la Mbulu, wakati wa Jubilei ya Miaka 25 ya Upadri wa Mhashamu Askofu Antony Lagwen. **PICHA: UTUMISHI**

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.
Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-27

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

Akiwa kwenye ofisi yake karibu na eneo la Makumbusho jijini Dar es Salaam, Boniphace Materu aliendelea kuvuta sigara zake mfululizo.

Kila kitu alichokifanya aliona chema. Utajiri wake ulizidi kuongezeka. Makampuni yake yaliendelea kuzalisha faida, wakati mwingine tofauti na alivyofikiria.

Gereji zake zilizidi kupata wateja, akiwa na tenda ya kutengeneza mabasi ya kusafiri yanayomilikiwa na vigogo ambao hawakutaka majina yao yawekwe hadharani na hata wafanyabiashara wenzake.

Mpango wake wa kuwania ubunge katika moja ya jimbo mkoani Kilimanjaro alikozaliwa nao ulikuwa ukiendelea vizuri. Alijiona mwenye bahati kwenye ulimwengu huu.

Siku yake ya mkononi iliita. Baada ya kuona jina alitabasamu kidogo, halafu akaiweka sikioni. "Niambie."

"Mkuu naomba unitumie milioni mbili kwa ajili ya kulainisha baadhi ya wapiga kura. Unajua wanakukubali sana, sema unajua tena wanataka chochote kitu. Hili jimbo ni lako tu mkuu." Sauti ilisikika upande wa pili.

Huyo alikuwa ni mpambe wake aliyemuweka kuhakikisha anafanya kila njia, wananchi wa jimbo hilo wanamchagua yeye kuwa mbunge mwakani.

"Haina neno, kuna kazi hapa naifanya, nikimaliza nikakucheki. Nitaitumia kwenye simu yako. Wewe fanya kazi, yaani nipata ubunge wewe mwenyewe utafurahi." Waliongea kiasi cha dakika mbili hivi hadi pale waliporidhika kuwa wameelewena.

Ni kweli Materu pamoja na utajiri wake alikuwa anataka ubunge ili kuendelea kujijengea heshima. Ana kila kitu, utajiri wa pesa, viwanda, makampuni, mahoteli, gereji, kwa sasa alichohitaji ni kinga ya uheshimiwa.

Ilikuwa ni saa 12:00 jioni alipotoka ofisini na kuelekea kwenye gari lake. Alikutana na walinzi kama kawaida. Akawasalimia na siku hiyo aliamua kuwapa chochote. Akaingiza mkono mfukoni na kutoka na noti mbili za shilingi elfu kumi na kuwapa. Aliingia kwenye gari lake, akawapungia mkono na kuwaaga.

Askari ambao walikuwa na zamu ya jioni walikuwa wakikutana na zawadi ya pesa hizo kutoka kwa Materu.

Kuna wakati mpaka walikuwa wakigombania kwenda kulinda zamu jioni ili kupata hizo pesa. Ingawa Materu alikuwa hazitoi kila siku, lakini alikuwa akifanya hivyo mara kwa mara kiasi cha kujijengea heshima na kupendwa na walinzi wengi.




**Walinzi walimtaja kuwa ndiye bosi mwenye huruma, heshima na adabu kwa wafanyakazi wa chini na kuwajali, kuliko bosi mwenye cheo au tajiri yoyote aliyepanga au kuwa na ofisi kwenye jengo lile lenye ghorofa 10 lililopo Makumbusho.**

Walinzi walimtaja kuwa ndiye bosi mwenye huruma, heshima na adabu kwa wafanyakazi wa chini na kuwajali, kuliko bosi mwenye cheo au tajiri yoyote aliyepanga au kuwa na ofisi kwenye jengo lile lenye ghorofa 10 lililopo Makumbusho.

Ukweli haikuwa hivyo. Materu alikuwa mjanja sana. Hiyo alifanya kama ulinzi kwake. Alijua kabisa kuwa walinzi wengi walijua vitu vingi sana. Walikamata watu, mali na vitu mbalimbali vya magendo. Waliwajua hata watu wabaya ambao wanataka kuwafanyia wenzao ubaya. Kuna wakati waliwazuia hata baadhi ya wafanyakazi waliokuwa wanakuja usiku ofisini kwa sababu zisizojulikana. Mtu anarudi ofisini saa mbili au tatu usiku wakati ofisi zimefungwa. Walinzi hawa wanawazuia kwa sababu walishaambiwa kuwa muda wa kuondoka ofisini ni saa 1:00 usiku, hakuna mfanyakazi yoyote kwenye jengo lile ataruhusiwa kurejea.

Hata hivyo siku zote waswahili wanasema penye udhia penyeza rupia. Wapo ambao wanazuiwa lakini wanatumia pesa kuwahonga. Na wanachofuata ofisini si kingine ila ni kuwafanyia wenzao ushirikina. Mtu anakuja ofisini kwa ajili ya kuweka hirizi, au kitu chochote alichopewa na mganga kwenye ofisini.

Kwa sababu hiyo, kuna wanaopewa taarifa za siri kuwa fulani alikuja jana usiku na kwenda kwenye ofisi yako, hivyo usiingie. Au fulani kafanya hivi, hivyo sehemu fulani kuwa nayo makini sana, au mtu fulani kuwa naye makini. Watu wanaopata taarifa mara nyingi huwa ni wale wanaowaachia chochote walinzi.

Materu alijifunza kitu kuwa mlinzi japo kuna baadhi ya wafanyakazi huwadharau kutokana na kazi zao za kukaa mlangoni, getini, kuuliza watu maswali, kufungulia geti magari, lakini ni watu muhimu kwenye ulinzi binafsi.

Kwa sababu, yoyote atakayefika pale na kumuuliza mtu ambaye humjali kwa kumuachia chochote kitu mara kwa mara, basi atapigwa maswali, halafu atawasiliana kwanza na mwenyewe kabla ya kumruhusu.

Hii imesababisha wengi kuepuka maadui zao, au watu ambao walikuwa wanataka kuja kuwadhuru.

Na hili ndilo limemfanya Materu awe hivyo. Anafanya hivyo kama kinga, kwani chochote kibaya kikitokea dhidi yake, watamtaarifu na yeye atajua jinsi gani ya kuepuka.

Siku ya pili alifanya hivyo hivyo. Lakini kabla hajapanda akawatania. "Naona mmepata mlinzi mwingine hapo." Walinzi waligeuka. Halafu wakaangua kicheko. "Rafiki yetu huyu, yupo wiki ya pili sasa, mara anapita mara anakaa jirani hapo. Ila siyo mgomvi. Anakaa mwenyewe anaongea maneno yasiyoeleweka, halafu huyo anaondoka." Akajibu mmoja wa walinzi.

Walikuwa wakimzungumzia mwendawazimu. Mita chache kutoka walipo, alikaa mwendawazimu mmoja aliyekuwa akila mikate mikavu. Kwake Materu ilikuwa ni mara ya kwanza kumwona, lakini kwa walinzi ilikuwa ni wiki ya pili. Ni kweli alikuwa akija pale, anasimama, mara anakwenda kukaa pembeni, na kuna siku anapita tu bila kusimama kama vile hapajui.

*ITAENDELEA JUMAMOSI*

# Mashabiki wasubiria dabi ya Majiji

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU mbili za Ligi Kuu zinazomikilikiwa na Halmashauri za Majiji, Pamba jiji na Dodoma Jiji, zitavaana leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza katika mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara, iliyoanza wiki iliyopita.

Mashabiki wa soka nchini wameipa jina mechi hiyo kuwa ni 'dabi ya majiji' kutokana na timu zote mbili kumililikiwa na majiji.

Pamba ambayo itakuwa mwenyeji, inamilikiwa na jiji la Mwanza, itaikaribisha Dodoma ambayo nayo inamilikiwa na jiji la Dodoma.

Pamba ambayo itakuwa nyumbani, itakuwa na kibarua cha kuhakikisha inapata ushindi wa kwanza kwenye Ligi Kuu mbele ya mashabiki wake, kwani katika mchezo wa kwanza ililazimishwa suluhu kwenye uwanja wa CCM Kirumba dhidi ya Prisons.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Bikhu Kutecha, amesema benchi la ufundi na wachezaji wamejiandaa vyema kwa ajili ya kuwapa furaha mashabiki wake baada ya kuikosa wiki iliyopita.

"Niwatake tu mashabiki wa soka Mwanza kumiminika kwa wingi kuishangilia Pamba ili ipate ushindi, tulikosa katika mechi ya ufunguzi, lakini walimu wameona makosa na wameyarekebisha, mpira una matokeo matatu, na huu ni mwanzo kabisa wa ligi, najua tutafanya vizuri," alisema Mwenyekiti huyo.

Meneja wa Dodoma Jiji, Charles Kombe, amesema lengo lao katika mchezo wa leo ni ushindi, na wao wanauhitaji zaidi baada ya kufungwa bao 1-0 dhidi ya Mashujaa FC, Jumamosi iliyopita, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

"Hakuna mpinzani yoyote anayekwenda katika mchezo akasema atafungwa, hivyo hata sisi tunakwenda kupambana kushinda, kama tukipoteza hayo yanakuwa ni moja tu kati ya matokeo ya mchezo.

Vijana wetu wana morali kubwa, bila kujali kama tumepoteza mchezo uliopita, kwa hiyo tunaahidi kuwa na mechi nzuri," alisema meneja huyo.

Katika msimamo wa ligi, Pamba iko katika nafasi ya nne na pointi moja, Dodoma ikishika nafasi ya 14, ikiwa haina pointi.

# SIMBA QUEENS KUIKABILI POLISI KENYA NUSU FAINALI

**Na Somoe Ng'itu**

SIMBA Queens itakutana na Polisi ya Kenya katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Mashindano ya Afrika Mashariki na Kati kwa Wanawake (CECAFA), itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Abebe Bikila ulioko Addis Ababa, Ethiopia.

Wawakilishi hao wa Tanzania wamemaliza wakiwa wanaongoza Kundi A wakati Maafande hao wa Kenya walimaliza nyuma ya vinara wa Kundi A, wenyeji CBE.

Simba Queens imemaliza hatua ya makundi ikiwa na pointi saba baada ya kupata sare ya mabao 2-2 dhidi ya PVB Buyenzi ya Burundi ambayo imeyaaga mashindano hayo.

PVB Buyenzi ndio ilikuwa ya kwanza kupata bao katika mchezo huo lakini mshambuliaji Mkenya wa Simba Queens, Jentrix Shikangwa alifanikiwa kusawazisha huku kiungo nyota Vivian Corazone akipachika goli la pili.

Nusu fainali nyingine ya mashindano hayo itawakutanisha CBE dhidi ya Kawempe Muslim Ladies ya Uganda wakati fainali itachezwa Agosti 29, mwaka huu.

Bingwa wa mashindano hayo atawakilisha CECAFA katika Fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake zitakazofanyika baadaye mwaka huu.

Mwaka jana Tanzania iliwakilishwa na JKT Queens lakini iliishia hatua ya makundi wakati msimu uliotangulia Simba Queens ilicheza hatua ya nusu fainali.




Wachezaji wa Timu ya Mpira wa Kikapu ya Vijana wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kocha Kagera Sugar aitisha Singida BS

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Paul Nkata, ametamba kuiadabisha Singida Black Stars kwa kuipa kichapo katika mchezo wa raundi ya pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa leo, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

Kocha huyo raia wa Uganda, amesema licha ya kwamba wanakwenda kucheza na timu kubwa, ngumu na yenye wachezaji bora kutoka mataifa mbalimbali ya nje, lakini anaamini kikosi chake kina uwezo wa kuwasimamisha na kupata ushindi.

"Tunajua tunakwenda kucheza na timu nzuri, ina wachezaji wengi kutoka nje ya nchi, imeshinda katika mchezo wa kwanza na sisi tunataka hapa nyumbani tuchukue pointi tatu za kwanza ili tukae sehemu nzuri, nawataka mashabiki wa mkoa huu, waje kwa wingi kuitazama na kuishangilia timu yao kwa sababu utakuwa ni mchezo wa kwanza kwao wa ligi kuuona msimu huu," alisema kocha huyo ambaye pia utakuwa ni mchezo wake wa kwanza kuiongoza timu hiyo kwenye ligi.

Utakuwa mchezo wa kwanza kwa Kagera, ambayo ratiba ilionyesha ingecheza mechi ya raundi ya kwanza dhidi ya Yanga wiki iliyopita, lakini uliahirishwa kutokana na wenzao kuwa kwenye michuano ya kimataifa.

Kocha Msaidizi wa Singida Black Stars, Denis Kitambi, amesema ingawa wanacheza ugenini, lakini wanataka kupata ushindi ili kuzoa pointi sita za ugenini.

Katika mchezo wa kwanza, ilishinda mabao 3-1 dhidi ya KenGold, ambao uliochezwa Uwanja wa Sokoine, Mbeya.

"Tulishinda mechi ya kwanza, lakini bado tulionekana kuwa na mapungufu, hasa ya kuruhusu mabao kirahisi, na ndilo tulilolifanyia kazi sana wiki hii, natumai mchezo utakuwa mzuri, tukishinda itakuwa safi sana, tutakuwa tumepata pointi sita ugenini," alisema.

Singida Black Stars inashika nafasi ya pili nyuma ya Simba, ikiwa na pointi tatu, huku Kagera Sugar ikiwa haina pointi na leo utakuwa mchezo wao wa kwanza.

## ZISIKUPITE

### STERLING APEWA OFA VILLA
WINGA wa Chelsea, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 29 amepewa ofa na Aston Villa, lakini Unai Emery hana uhakika kama mshambuliaji huyo wa England atafaa katika mipango yake. ***(Mirror)***

### AYEW AKARIBIA LEICESTER
KLABU ya Leicester City inakaribia kumnunua mshambuliaji wa Crystal Palace mwenye umri wa miaka 32, Jordan Ayew. ***(Sky Sports)***

### ...WATATU KWENYE RADA
WACHEZAJI wengine wawili wa kiungo cha kati pia wako kwenye orodha ya kocha wa Leicester, Steve Cooper kabla ya dirisha kufungwa. ***(Telegraph)***

### REINIER AWANIWA N'CITY
KLABU ya Norwich City imejitokeza kuwania saini ya kiungo mshambuliaji wa Brazil, Reinier mwenye umri wa miaka 22 kutoka Real Madrid. ***(O Globo)***

### PHILLIPS KWA MKOPO STOKE
KLABU ya Tottenham Hotspur inatazamiwa kumruhusu beki wa kati mwenye umri wa miaka 19, Ashley Phillips kujiunga na Stoke kwa mkopo. ***(Athletic)***

### WATFORD KUMUUZA ASPRILLA
GIRONA imekubali dili la awali la pauni milioni 21.2 pamoja na nyongeza kutoka kwa Watford kwa ajili ya kumnunua kiungo wa Colombia, Yaser Asprilla mwenye umri wa miaka 20. ***(Sky Sports).***

### MATS HUMMELS AGOMBEWA
KLABU za Brighton, Real Sociedad na Real Mallorca zinapigania kumsajili beki wa Ujerumani, Mats Hummels mwenye umri wa miaka 35 kwa uhamisho wa bila malipo. (***Florian Plettenberg***)


### CHIESA AKARIBIA KUTUA BARCA
BARCELONA imekubali makubaliano ya binafsi na winga wa Italia, Federico Chiesa mwenye umri wa miaka 26, ambaye anatarajiwa kununuliwa kwa pauni milioni 11 kutoka Juventus. ***(Sport)***

### TATU ZAMUWINDA KIERAN TRIPPIER
EVERTON, AC Milan, Bayern Munich na klabu kadhaa nchini Uturuki zina nia ya kumsajili beki wa Newcastle, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 33. ***(Talksport)***

### NUNES ATAKIWA BRENTFORD FC
KLABU ya Brentford iko tayari kukamilisha dili la pauni milioni 10 kwa winga wa Brazil, Gustavo Nunes mwenye umri wa miaka 18 kutoka Gremio. ***(Fabrizio Romano)***

### JOHN EGAN ANUKIA BURNLEY
BEKI wa Jamhuri ya Ireland, John Egan mwenye umri wa miaka 31 anafanya mazoezi na Burnley baada ya kuondoka Sheffield United. ***(Football Insider)***

## DOND A SOKA MAGA A ULAYA



# COURTOIS AKATAA KUICHEZEA UBELGIJI

●●●Ameweka wazi kuwa hatorejea kwenye timu hiyo ikiwa kocha wa sasa....

**MADRID, Hispania**

GOLIKIPA wa Real Madrid, Thibaut Courtois amesema katika chapisho lake kwenye mtandao wa kijamii Alhamisi, kwamba hatarejea katika timu ya taifa ya Ubelgiji kama kocha wa sasa, Domenico Tedesco ataendelea kuinoa timu hiyo.

Courtois, ambaye alikosa sehemu kubwa ya msimu uliopita baada ya kupata majeraha mawili ya goti, aliachwa kwenye kikosi cha Ubelgiji kilichoshiriki Euro 2024 licha ya kuanza kuichezea Real Madrid kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kwa bahati mbaya, kufuatia matukio na kocha na baada ya kutafakari sana, nimeamua kutorejea katika timu ya taifa ya Ubelgiji chini ya usimamizi wake," aliandika Courtois, ambaye amecheza Ubelgiji mara 102.

"Katika suala hili, ninakubali sehemu yangu ya wajibu. Hata hivyo, nikitazama mbele, ukosefu wangu wa imani kwake haungechangia katika kudumisha hali ya lazima ya ukarimu."

Courtois alitofautiana hadharani na Tedesco mwaka jana baada ya kuondoka kwenye kikosi cha Ubelgiji kabla ya mechi ya kufuzu kwa Euro 2024 huku kukiwa na mzozo wa kutochaguliwa kurithi mikoba ya Eden Hazard kama nahodha.

Tedesco alisema Courtois aliondoka ghafla kambini baada ya kutojisikia heshima ndani ya timu, lakini Courtois alikanusha madai ya Tedesco na kusema aliondoka kambini kutokana na tatizo la goti.

"Shirikisho, ambalo nimekuwa na majadiliano nalo mara kadhaa, linakubali msimamo wangu na sababu ambazo zilinipeleka kwenye uamuzi huu mchungu lakini thabiti," aliongeza Courtois.

"Ninajuta kuwakatisha tamaa baadhi ya mashabiki, lakini nina hakika kwamba hii ni hatua bora zaidi kwa Ubelgiji, kwani inafunga mjadala na kuruhusu timu kuzingatia malengo yake."

Ubelgiji ilitolewa na Ufaransa katika hatua ya 16 bora kwenye Euro 2024, huku kipa wa Al Qadsiah, Koen Casteels akianza michezo yao yote minne.

# DYBALA AKATAA MAMILIONI YA SAUDIA, KUBAKI ROMA

**ROME,** ITALIA

NYOTA wa Argentina, Paulo Dybala ametangaza kwamba atasalia na AS Roma, na kumaliza wiki za uvumi zinazomuhusisha na uhamisho wa kuhamia klabu ya Saudi Pro League ya Al Qadsiah.

Ripoti nyingi zinaonesha kwamba Dybala alikataa ofa ya euro milioni 75 kwa mkataba wa miaka mitatu.

"Asante Roma...Tuonane Jumapili," alisema kwenye chapisho lake kwenye mtandao wake wa kijamii wa Instagram.

Uamuzi wa Dybala ulikuja huku kukiwa na hali ya sintofahamu kuhusu mustakabali wake.

Alifanya mazoezi tofauti na kikosi cha kwanza cha Roma Alhamisi na hakuwepo kwenye kikosi cha kwanza kwenye mechi yao ya ufunguzi ya Serie A dhidi ya Cagliari Jumapili iliyopita.

Dybala anaingia mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake na Roma lakini mkataba huo unaongezwa moja kwa moja ikiwa atacheza angalau mechi 15 rasmi msimu huu.

Atapata euro milioni 7.5 pamoja na euro milioni 2 katika nyongeza na bonasi.

Tangu ajiunge na Roma kutoka Juventus mwaka 2022, Dybala amejidhihirisha kama mtu muhimu katika timu hiyo. Katika mechi 78, amefunga mabao 34 na kutoa asisti 18.

Mashabiki wa Roma walikuwa wameweka wazi hisia zao wiki iliyopita, huku maandamano nje ya uwanja wa mazoezi ya klabu hiyo yakiitaka klabu hiyo kutomuhamisha nyota huyo.

Kujitolea kwa Dybala kwa Roma kulizua shangwe miongoni mwa mashabiki ambao walikusanyika nje ya nyumba yake Alhamisi usiku kusherehekea habari hizo.

Al Qadsiah, ambayo ilijaribu mara nyingi kupata huduma ya Dybala tangu mwanzoni mwa dirisha la usajili la majira ya kiangazi, ni klabu mpya ya Saudia iliyopandia daraja na yenye orodha ya nyota wengi akiwemo mlinzi wa zamani wa Real Madrid, Nacho Fernandez na mshambuliaji wa zamani wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang.

Uamuzi wa Dybala kusalia ulipokelewa na shangwe kutoka kwa mchezaji mwenzake wa Roma na Argentina, Leandro Paredes. "Kwa wale ambao hawajaelewa, anabaki nasi," aliandika.




## Dest afurahia matarajio ya Pochettino kuinoa Marekani

**AMSTERDAM,** UHOLANZI

MLINZI wa Marekani, Sergiño Dest alisema anafurahishwa na uwezekano wa kuwasili kwa Mauricio Pochettino kama kocha wa timu yao ya taifa ya wanaume.

Dest, ambaye aliumia goti Mei na huenda akakaa nje hadi mwaka 2025, alisema anafikiri kuwasili kwa kocha huyo wa Argentina kunaweza kuwa msaada mkubwa kwa timu hiyo.

"Ndio, inasisimua," alisema akiiambia ESPN wakati akihudhuria mashindano ya 'Formula One' ya Uholanzi Grand Prix wikendi hii.

"Ni wazi, amekuwa kocha wa watoto wakubwa na ni kocha anayejulikana. Hiyo itakuwa uzoefu mzuri wa kufanya mazoezi chini yake.

Pochettino amejijengea sifa ya kuwakuza wachezaji hasa wakati alipokuwa Tottenham Hotspur kuanzia 2014 hadi 2019.




"Hiyo inasisimua. Tutaona na tunatumaini inaweza kutusaidia sote ...., kuwa na matokeo bora kabisa kwenye Kombe la Dunia la 2026, unajua? Kwa sababu sisi tutakuwa wenyeji," aliongeza Dest.

"Tunahitaji kuchukua hatua kwa hatua kwa sababu bado haypo."

Dest alisema anatumaini habari hiyo Itakuwa rasmi hivi karibuni.

Marekani ina mechi mbili za kirafiki wakati wa dirisha la kimataifa la Septemba dhidi ya Canada na Panama Septemba 7 na Septemba 10.

Chanzo kiliiambia ESPN kwamba kocha msaidizi wa zamani, Mikey Varas atachukua jukumu la kuiongoza Marekani kwa mechi hizo mbili.

ESPN iliripoti wiki iliyopita kwamba Pochettino amekubali kurithi mikoba ya Gregg Berhalter kama kocha wa Marekani na sasa zinasubiriwa taratibu rasmi kukamilisha mpango huo.

Anatarajiwa kuinoa timu hiyo kwa mara ya kwanza dhidi ya Mexico katika mechi ya kirafiki itakayofanyika Uwanja wa Akron huko Guadalajara, Oktoba 15.

## Arsenal yamtwaa Merino, Nketiah atimkia Forest

**LONDON,** ENGLAND

ARSENAL imefikia makubaliano ya msingi ya kumsajili Mikel Merino kutoka Real Sociedad na wako ukingoni kukamilisha mpango wa kumruhusu Eddie Nketiah kujiunga na Nottingham Forest, vyanzo vimeiambia ESPN.

Kikosi hicho cha London Kaskazini kinatarajia kulipa ada ya awali ya pauni milioni 28 pamoja na nyongeza ya takriban pauni milioni nne ili kumsajili Merino ambaye atakuwa mchezaji wa tatu kusajiliwa katika klabu hiyo msimu wa majira ya joto baada ya David Raya kwa mkopo kutoka Brentford na Riccardo Calafiori aliejiunga nao kutoka Bologna.

Merino sasa anatarajiwa kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu na vyanzo vimedokeza kuwa anatarajiwa kusaini mkataba wa miaka minne na chaguo la mwaka mmoja zaidi.

Mazungumzo pia yameendelea na Forest kuhusu Nketiah, huku chanzo kimoja kikipendekeza klabu hiyo ya Midlands imetoa ofa iliyoboreshwa ya takriban pauni milioni 30 pamoja na nyongeza ambazo Arsenal iko tayari kukubali.

Chanzo hicho kiliongeza kuwa bosi wa Forest, Nuno Espirito Santo alizungumza na Nketiah ili kumpa uhakikisho kuhusu muda wake wa kucheza kwenye Uwanja wa City Ground.

Arsenal ilikanusha mikataba yote miwili ilihitimishwa ilipowasiliana na ESPN.

Lakini vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Mikel Arteta amesukuma dili hilo kibinafsi.

Merino alijiunga na Sociedad Julai 2018 na amefunga mabao 27 katika michezo 242 aliyoichezea klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 amebakiza mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake uliopo na alikataa pendekezo la klabu hiyo ya LaLiga la kuongeza muda.

Merino alicheza katika mechi zote saba za Hispania ikishinda Euro 2024, na kuwalaza England katika fainali mwezi uliopita.

Nketiah bado hajakamilisha makubaliano binafsi, lakini vyanzo vinasema kuna matumaini kwamba hatua yake itakamilika katika siku zijazo.

***

HABARI MICHEZO

# 'UGENI' WASUMBUA WACHEZAJI SIMBA

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Simba imewataka wanachama na mashabiki wao kuwavumilia na kuwapa muda wachezaji wapya wa kigeni waliosajiliwa msimu huu kwani wengi wao wanasumbuliwa na ugeni, tofauti na wale wapya ambao wamesajiliwa msimu huu kutoka klabu za hapa nchini.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema wachezaji wa Kitanzania ambao usajili wao wengi waliuona wa kawaida tu, wameonekana kuibeba zaidi timu hiyo katika mechi za mwanzo tofauti na wageni ambao hakuna kingine kinachowasumbua zaidi ya ugeni tu.

Alisema hayo kufuatia wengi kuhoji wachezaji wa kigeni waliosajiliwa kuonekana hawajachangamka, tofauti na wachezaji wapya wa Kitanzania ambao usajili wao haukuwa na mbwembwe.

„Timu yetu haijakaa sawa, tunashinda lakini si kwa namna ya kufurahisha, tunashinda kwa sababu ya juhudi za wachezaji na mbinu za walimu, lakini si ushindi wa urahisi, na hii inatokana na ugeni wa wachezaji wetu, kwa hiyo wanachama na mashabiki ni lazina wawe na subira, lakini naona taratibu wanaanza kuzoeana, watazoea ligi hivi karibuni na wataizoea Tanzania,“ alisema Ahmed.

Alisema wachezaji wa Kitanzania wanaonekana wamechangamka zaidi kwa sababu wanacheza ligi ambayo wameizoea katika mazingira yale yale, licha ya kwamba wamekuja kwenye timu mpya, ndiyo maana hawajaathirika na ugeni.

„Muangalie Valentino Mashaka, mechi ya kwanza ameshatufungia bao, Awesu Awesu naye akiwa ametokea benchi tu akafunga bao la tatu dhidi ya Tabora United katika mechi yetu ya Ligi Kuu Jumapili iliyopita, yule Addulrazack Hamza ndiyo balaa.

Zamani tulikua tunajua beki wa kati lazima utumie nguvu nyingi, lakini Hamza anatufundisha kuwa beki wa kati anaweza akatumia akili na akafanya kazi yake kwa ubora wa hali juu, yaani kama hakabi vile kumbe ndiyo anapokonya mali anaondoka,“ alisema Ahmed.

Valentino, alisajiliwa kutoka Geita Gold, Awesu kutoka KMC na Hamza kutoka SuperSport ya Afrika Kusini, lakini beki huyo wa Kitanzania, ana uzoefu na soka la Bongo kwani aliwahi kuzichezea klabu za KMC, Mbeya City na Namungo kabla ya kutimkia Afrika Kusini.



Mratibu wa mashindano ya soka ya Ulinzi Cup yanayoratibiwa na Jeshi la Polisi Mkoani Tanga, Sophia Wakati, akisalimiana na wachezaji wa timu ya Majengo FC ya Pongwe kabla ya kuanza mchezo wa mashindano hayo uliochezwa uwanja wa Ziwani Pongwe juzi na kumalizika kwa Chote FC kuibuka na ushindi wa bao 1-0. **PICHA:OSCAR ASSENGA**

# Ibrahim aweka rekodi KenGold FC

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kufungwa mabao 3-1 dhidi ya Singida Black Stars, katika mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu, timu ya KenGold, imemuweka mchezaji wao Joshua Ibrahim kwenye vitabu vya kumbukumbu ya klabu hiyo kwa kufunga bao la kwanza katika mchezo wao kwa kwanza wa ligi.

Katika taarifa yake, klabu hiyo imesema kuwa Joshua amewekwa kwenye rekodi kuwa ndiye mchezaji wa kwanza kufunga bao la kwanza katika mechi ya kwanza ya Ligi Kuu katika hitoria ya klabu hiyo.

„Goli letu la kwanza kwenye historia ya klabu yetu baada ya kupanda Ligi Kuu, limefungwa na Joshua, na ndiyo linakuwa la kwanza kufungwa tangu tumepanda daraja na kushiriki Ligi Kuu, anaingia kwenye vitabu vya kumbukumbu vizazi hadi vizazi,“ ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Mechi hiyo ilichezwa Jumapili iliyopita kwenye uwanja wa Sokoine, Mbeya, na KenGold kuambulia kipigo cha mabao 3-1.

Lakini pamoja na kufungwa, klabu hiyo imesema rekodi ya mchezaji huyo haitofutika, hivyo wameamua kuitambia kwani atakuwa amefungua njia kwa wenzake.

Timu hiyo inayomilikiwa na mfanyabiashara Keneth Mwakyusa inatararajia kushuka tena dimbani, Septemba 11 kucheza dhidi ya Fountain Gate.

# Yanga kumaliza kazi mbele ya Vital O

INATOKA UK. 24

mbele ya Yanga leo.

Katika hatua nyingine, kikosi cha Azam FC nacho leo kinaingia uwanjani jijini Kigali, Rwanda kwa ajili ya mchezo wa marudiano dhidiya APR ya nchini humo.

Azam wanaingia uwanjani wakiwa mbele kwa bao 1-0 kufuatia ushindi walioupata katika mchezo wa kwanza uliochezwa wiki iliyopita kwenye uwanja wa Azam Complex.

Kikosi hicho cha 'Wanarambaramba' hao wanahitaji ushindi wowote au matokeo ya sare kuweza kusonga mbele kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa wa Afrika.

# Simba SC yaridhishwa viwango nyota wa kigeni

INATOKA UK. 24

timu na tuanze upya, wachezaji tuliokuwa nao walishapungua viwango, wasingeweza kutusaidia tena, pili morali yao ilikuwa imeshuka, tatu umri wao ulikuwa mkubwa, wasingeweza kufanya maajabu mengine, hata kama wangekuwa wanataka kufanya kitu, lakini mambo hayo matatu yalikuwa yanawazuia, umri, moyo wa kupambana, na ubora ulikuwa umeshuka, tukaamua bora tufagie na kuleta wengine ambao ndiyo hawa na wanaonyesha mwanga mkubwa siku za mbele,“ alisema.

Wakati wengi wanaona imesajili wachezaji wengi, Meneja Habari huyo alisema wao wanaona wamesajili wachache kwani walitaka kusajili zaidi ya 15, lakini baadaye wakaona ni lazima wabakishe wenye uzoefu kwenye kikosi na Ligi Kuu.


Simba kesho itashuka uwanjani kucheza mchezo wao wa pili wa Ligi Kuu dhidi ya Fountain Gate.

Mchezo huo utachezwa kwenye uwanja wa Manispaa ya Kinondoni, Mwenge jijini Dar es Salaam pia ukiwa mchezo wa kwanza kwa Fountain Gate msimu huu.

Michezo
Jumamosi Agosti 24, 2024
Nipashe

## Courtois akataa kuichezea Ubelgiji

UKURASA 21



# Yanga SC kumaliza kazi mbele ya Vital O

### ●●●Kocha Gamondi aweka wazi, kazi haijaisha mpaka baada ya dakika 90, Azam nayo...

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA wa klabu yaYanga, Miguel Gamondi, amesema licha ya kuwa mbele kwa mabao 4-0 dhidi ya wapinzani wao wa leo, Vital O ya Burundi kwenye mchezo wa mzunguko wa pili hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, bado kazi yao haijaisha mpaka baada ya dakika 90.

Yanga walipata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya wapinzani wao hao kwenye mchezo wa kwanza wiki iliyopita uliochezwa kwenye uwanja wa Azam Complex na leo wanarudiana kwenye uwanja huo.

Gamondi, alisema licha ya kuwa mbele kwa ushindi huo, bado hawatawadharau wapinzani wao hao katika mchezo wa leo utakaochezwa saa 1:00 usiku.

„Huwa sipendi kusikiliza mpinzani anawaza au kuongea nini mara nyingi natumia muda wangu kuandaa timu yangu kuwa bora, timu yangu ina wachezaji bora hivyo sina wasiwasi na mchezo huo, lakini lazima tuchukue tahadhari na kutowadharau wapinzani wetu licha ya kuwa mbele," alisema Gamondi.

Alisema ana matumaini makubwa na wachezaji wake kutokana na mbinu alizowapa ili kujilinda na kushambulia dhidi ya wapinzani wao hao ambao anaamini watarudi na nguvu mpya.

"Bado mchezo hatujamaliza, kuna dakika 90 nyingine, tutakuwa makini sana kwenye kumaliza mchezo huu, tupo tayari kwa mchezo," alisema Gamondi.

Aidha, golikipa, Abutwalib Mshery ambaye alizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake alisema wamefanya maandalizi ya kutosha na kwa kufuata maelekezo waliyopewa na kocha wao katika uwanja wa mazoezi.

"Hatuwadharau wapinzani wetu kwa sababu tutumeshinda mechi ya kwanza, mchezo wa leo tutaingia kama tunaanza upya mashindano haya lakini pia hamasa ya goli la Mama (Rais Samia) inaongeza chachu ya kufanya vizuri zaidi," alisema Mshery.

Kwa upande wake kocha wa Vital' O, Sahabo Parris aliesema mechi ya kwanza waliku wawanaitizama na kuangalia namna ya kuwafunga Yanga na walicheza vizuri lakini haikuwa bahati kwao.

Alisema anaimani kubwa na timu yake kufanya vizuri na kuweza kuwapa ushindani mkubwa Yanga zaidi ya mechi iliyopita.

"Ninaimani kubwa na wachezaji wangu, tumejiandaavizurinaushindiupo, tunaweza kurudisha mabao manne, huu ni mpira na lolote linaweza kutokea," alisema Parris.

Nahodha wa timu hiyo, Ndayishimiyie Hussein, alisema mchezo uliopita walifungwa na wapinzani wao kwa kuwa hawakutumia vizuri nafasi zao.

Alisema wamejipanga na wamefanyia kazi mapungufu yao na wapo tayari kutoa ushindani

INAENDELEA UK. 23



## Simba SC yaridhishwa viwango nyota wa kigeni

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikijiandaa na mchezo wa raundi ya pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara hapo kesho, klabu ya Simba imesema imeridhishwa na kiwango cha wachezaji wao wote wapya iliyowasajili ikiamini watawapa mafanikio makubwa.

Uongozi huo umesema walifanya jambo la msingi kuondoa baadhi ya wachezaji na kuleta wachezaji wapya na kama wasinge fanya hivyo kusinge kuwa na uhakika wa kufanya vizuri msimu huu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema wachezaji wengi ambao imewaacha walikuwa wameshuka viwango, hawakuwa na moyo wa kupambana na umri ulikuwa umewatupa mkono.

Ahmed, alisema usajili walioufanya ni kwa ajili ya kutengeneza kikosi kipya kitakachorudisha heshima na furaha ya mashabiki na wanachama wa klabu hiyo.

Alisema wana matumaini makubwa na wachezaji waliowasajili msimu huu kwani ni vijana wenye umri mdogo ambao wanahitaji kufanya vizuri kwenye tasnia ya soka ili wasonge mbele, na wana moyo wa kujituma.

"Wachezaji tulionao msimu huu uwezo wao na ubora unapanda juu, tofauti na walioondoka ambao walikuwa wanashuka, na kwa mfano tungesema tusiwaondoe, msimu huu ulioanza ungekuwa mgumu zaidi na uwenda tungemaliza kwenye nafasi mbaya zaidi ya msimu uliopita,"alisema Ahmed na kuongeza.

"Simba ilikuwa lazima tuvunje

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >